epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Machi 28, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581629
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 8

**MAJALIWA AAGIZA TAMISEMI IJIFUNZE KWA NMB KUTUNZA YATIMA**



# Askofu Bagonza aibua uvundo wa mafarakano

• **Adai** uko serikalini hadi kanisani; apendekeza mambo manne... *Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wafanyakazi katika Bandari ya Mwanza Kusini, wakishuhudia kuanza kwa safari za majaribio ya meli kubwa ya MV. Mwanza 'Hapa Kazi Tu' jana. Meli hiyo itazunguka kwa siku tatu katika maeneo ya visiwa vya Mkoa wa Mwanza, ili kupima ufanisi wake. Ina uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo pamoja na magari madogo 20 na malori matatu. **Habari Uk. 10**. **PICHA: VITUS AUDAX**

UKURASA WA 2
**MVUA YABOMOA KM 60 BARABARA MIKOA MINNE**

UKURASA WA 2
**WAZIRI BITEKO ASIMAMISHA KAZI MENEJA MKUU KAMPUNI YA UMEME**



UKURASA WA 5
**TGNP YAIBUA HOJA BAJETI JUMUISHI KWA MAKUNDI YOTE**

CAG UTOUH AJA NA HATUA:

# Itungwe sheria ya ubadhirifu wa fedha serikalini

**Na Ludovick Utouh**

Kupitia sheria hii, serikali ipunguze hatua za kiutawala/kinidhamu za kushughulikia vitendo hivi, badala yake iweke hatua za kisheria mahsusi za kushughulikia wahusika wa vitendo hivyo vya ufisadi dhidi ya fedha na rasilimali...

UKURASA 4

# Shinikizo la juu la damu janga, JKCI yafichua hali mbaya



UKURASA 8

**MICHEZO** **YANGA: TUTAISHANGAZA AFRIKA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Waendesha pikipiki maarufu Bodaboda, wakipita katikati ya barabara ya mabasi ya mwendokasi katika eneo la Kimara Baruti, jijini Dar as Salaam jana, bila ya kujali kuwa wanavunja sheria. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Askofu Bagonza aibua uvundo wa mafarakano

**Na Restuta James**

ASKOFU Dk. Benson Bagonza wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, ametoa salamu za Pasaka, akilalamika kumea uvundo wa mafarakano serikalini hadi kanisani.

Kutokana na hali hiyo, Askofu Bagonza amependekeza kuwapo suluhisho la upatanisho kwa njia ya kufungua milango ya kuvumiliana, kubadilika na kujenga upya palipoharibika, huku kanisani akielekeza taasisi zake kuua alichokiita "Moshi wa chuki kuliko upendo".

Katika salamu zake hizo za Pasaka zilizo kwenye ukurasa mmoja wenye aya tano, Askofu Bagonza anataja mambo manne yanayohitaji kufanywa na mihimili ya Bunge, Serikali na Mahakama, huku akitaja upatanisho kama msingi wa Tanzania kustawi.

Askofu huyo katika salamu hizo alizozitoa jana, zikiongozwa na neno kutoka kitabu cha Walawi 16:29-30, Dk.Bangoza alisema nchi inahitaji upatanisho ili kufungua milango ya kuvumiliana, kubadilika na kujenga upya palipoharibika. Neno alilonukuu Askofu Bagonza kutoka Kitabu cha Walawi 16:29-30, linasema: "Hili ni sharti ambalo mnapaswa kulifuata milele: Siku ya 10 ya mwezi wa saba, ninyi wenyewe na hata wageni wanaoishi miongoni mwenu, ni lazima mfunge siku hiyo na kuacha kufanya kazi. Mtafanya hivyo kwa sababu siku hiyo ndiyo siku ambayo mtafanyiwa ibada ya upatanisho, msafishwe dhambi zenu, nanyi mtakuwa safi mbele ya Mwenyezi-Mungu."

Katika salamu zake, Askofu Bagonza anasema: "Kila eneo katika taifa letu kuna uvundo wa mafarakano. Mihimili karibu yote-Bunge, serikali na mahakama kumejaa mafarakano na kuishi kwa tahadhari kubwa na hofu ya kuwindana. Ndani ya taasisi za dini kuna moshi wa chuki kuliko upendo. Mwathirika mkuu wa mafarakano haya ni mpendwa wetu haki.

"Hatuwezi kutenda wala kusimamia haki ikiwa uamuzi wetu umejaa hila, chuki, ubinafsi, rushwa, visasi na kuongozwa na itikadi, dini na makundi maslahi."

Dk. Bagonza ambaye ni mwanafalsafa na mchambuzi wa masuala mbalimbali ya kisiasa na kijamii, anasema Kristo anayeadhimishwa mateso, kifo na ufufuko wake, alitumika kupatanisha wanadamu na Mungu na kati ya mtu na mtu.

"Asiyekubali kupatanishwa hawezi kupatanisha wengine. Asiyepatanishwa na wengine wala kuwapatanisha wengine, amefarakana na Mungu. Upatanisho unawezesha kufungua milango mingine kufunguka. Milango hiyo ni kuvumiliana, kubadilika na kujenga upya palipo haribika.

"Agano jipya na la kale yanakubaliana kwamba damu (eshagama), ni alama ya ukombozi na upatanisho. Damu isiyo na hatia isipokomboa inalaani. Damu ya Bwana Yesu ilikomboa na kutupatanisha na Mungu. Kwa kuwa haikuwa na hatia, walioimwagwa wanaalikwa kupatana na Mungu ili kuiepuka laana. Wanaoendelea kumwaga damu isiyo na hatia wanaalikwa kutubu na kupatanishwa na Mungu," anasema.

Askofu Bagonza anaongeza kuwa: "Mienendo yetu isiyofaa kama rushwa, matumizi mabaya ya madaraka, ukatili dhidi ya watoto, ukatili dhidi ya mazingira, udini, itikadi, biashara ya kuuza na kununua haki na dhulma dhidi ya taifa letu vinatokana na roho za mafarakano zinazokataa upatanisho.

"Kristo amefufuka, ninawasihi mpatanishwe. Rudini meza ya mapatano na madhabahu za kupatanishwa kwa sababu amri hii ni ya milele," Askofu Bagonza anahitimisha salama zake.

Wakristo nchini wanaungana na wenzao duniani kuadhimisha Pasaka kuanzia kesho (Ijumaa Kuu) hadi Jumatatu (Jumatatu ya Pasaka).

# Mvua yabomoa barabara inayounganisha mikoa minne

**Na Guriani Adolf,**
SUMBAWANGA

MVUA kubwa iliyonyesha mfululizo mwishoni mwa wiki iliyopita, imesababisha kukatika kwa mawasiliano ya barabara yenye urefu wa kilometa 60 na ukosefu wa huduma katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe na Tabora.

Kutokana na athari hizo, serikali imetoa Sh. billioni tatu za dharura kwa ajili ya kukarabati na kurejesha mawasiliano katika madaraja manne yaliyokatika kwenye Bonde la Ziwa Rukwa, wilayani hapa.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Nyakia Chirukile, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wakazi wa kata ya Ilemba alipokuwa katika ziara ya kukagua madhara yaliyotokea katika bonde hilo.

Licha ya kuharibu miundombinu na ukosefu wa huduma muhimu, mvua hiyo pia imesababisha kifo cha mtu mmoja huku nyumba nyingi zikibomoka. Pia madaraja kadhaa yamesombwa kutokana na mvua hiyo.

Alisema serikali kuu imetoa fedha hizo na kukabidhi Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) ambayo ndiyo yenye dhamana ya kujenga na kukarabati barabara za vijijini na wakati wowote itaanza kazi hiyo ili kurejesha mawasiliano katika baadhi ya vijiji.

"Napenda kuwafahamisha wakazi wote wa bonde la Ziwa Rukwa kuwa serikali inaziona na kuzitambua changamoto mnazopitia. Imetoa fedha za dharura kiasi cha Sh. billioni tatu ili TARURA wafanye ukarabati wa barabara na madaraja yaliyobomoko ikiwamo kujenga mengine mapya ili maisha yaendelee," alisema.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Rukwa, Mhandisi Mgeni Mwanga, alisema madaraja yote ambayo yako chini ya TANROADS tayari yameshaanza kufanyiwa marekebisho na kazi hiyo inafanyika usiku na mchana ili yaanze kupitika kwa kuwa mkandarasi yuko katika maeneo hayo. Alisema lengo ni kuhakikisha mawasiliano yanarejea katika muda mfupi ili kuondoa kero kwa wananchi wa bonde hilo.

Pia alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali imeshatumia zaidi ya Sh. bilioni tisa kwa kuwa kila kipindi cha masika, imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kukarabati na kurejesha mawasiliano kutokana na mvua kuharibu miundombinu ya barabara kila msimu wa masika.

Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Sakalilo, Farida Tandala, aliomba serikali kufanya upesi kujenga barabara na madaraja yaliyobomoko kwa kuwa wanapata tabu ya mawasiliano na kushindwa kupata huduma kwa baadhi ya bidhaa muhimu kutokana na magari kutofika katika vijiji vyao.

# Biteko amsimamisha kigogo kampuni ya umeme

**Na Benny Kingson,**
TABORA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Fulcheshmi Mramba, kumsimamisha kazi Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ujenzi wa Miundombinu, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme (ETDCO), Mhandisi Mohamed Abdallah, kwa kushindwa kusimamia vyema majukumu yake.

Dk. Biteko alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ukaguzi wa mradi wa kituo cha kupoza umeme cha Uhuru na kuonyesha kutokuridhishwa na utekelezaji wake kutokana na laini ya umeme kutoka Tabora hadi Urambo (kilometa 115) kuwa asilimia 10 tu.

ETDCO ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inasimamia utekelezaji huku ujenzi wa kituo cha kupoza umeme unaofanywa na kampuni ya TBEA kutoka China imetekeleza kwa asilimia 84.

Kutokana na kusuasua kwa ujenzi wa laini hiyo, Dk. Biteko aliagiza Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO kumwondoa Mhandisi Abdallah ambaye ameonekana kutotoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayosimamiwa na kampuni hiyo.

"Septemba 17, 2023 nilimtuma Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, kukagua mradi huu ambaye aliwapa maelekezo ya kukamilisha. Pia nilimtuma aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Meja Jenerali Paul Simuli, kuja kukagua mradi huu Desemba 17, 2023. Naye alitoa maelekezo ambayo hayajatekelezwa.

"Hatari iliyopo hapa ni kuwa TBEA atakamilisha kazi mapema Juni lakini umeme bado hautapatikana kwenye kituo kwa sababu laini ya umeme itakuwa haijakamilika," alisema Dk. Biteko.

Naibu Waziri Mkuu aliongeza kuwa kutokukamilika kwa wakati kwa laini ya umeme kutoka Tabora hadi Urambo, kutasababisha serikali kuilipa TBEA gharama za kuwapo eneo la mradi bila kazi ambayo ni asilimia 0.2 ya gharama za mradi, hivyo kuisababishia hasara serikali.

Alisema TBEA na ETDCO zote zililipwa malipo ya awali ya utekelezaji wa kazi kwa asilimia 50 lakini ETDCO inatekeleza kazi kwa kusuasua huku TBEA ikifanya kazi kwa wakati.

Biteko alsiema meneja mkuu huyo ameendelea kufanya kazi kwa mazoea na kusababisha kuchelewa kwa usambazaji wa nguzo na mpaka sasa zimepelekwa nguzo za umeme katika mradi wa ujenzi wa kituo hicho kwa asilimia 10 pekee wakati kazi imefikia asilimia 84 tofauti na matarajio.

"Hata hapa amemtuma mwakilishi huyo ni 'size' yangu. Katibu Mkuu tafuteni meneja mwingine huyo hafai. Sitataka mazoea na mtu wala kampuni yoyote na lazima tuheshimiane katika kazi. Kuna udhaifu mkubwa mwingi tu tu nimeyasikia, uswahili mwingi na wizi ndani yake," alisema.

Ujenzi wa kituo hicho utakaogharimu Sh. Sh.bilioni 40 hadi kukamilika, utawezesha maeneo mengine kupata huduma ya umeme na kwamba vituo vingine vimejengwa Sikonge eneo la Ipole kimefikia asilimia 89, Mlele aslimia 87 na Mpanda mkoani Katavi asilima 90 ikiwa mistari asilima 47 imekwishajengwa na ni kilometa 393 kutoka Tabora.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Athanas Nangali, alisema mradi wa ujenzi wa kituo hicho una msukumo wa umeme wa kilovati 132 kutoka Shinyanga hadi Tabora. Aidha, Dk. Biteko aliitaka kampuni ya ETDCO kujitathmini katika utekelezaji wa miradi yake kutokana na miradi mingi kusuasua pamoja na kutathmini utendaji wake wa kazi ndani ya menejimenti ambao si wa kuridhisha.

Naye Mhandisi Sosipeter Mlalo wa shirika hilo, alisema kituo hicho kitapokea KV 132 na kitakuwa na transfoma yenye uwezo wa MW 35 na kwa sasa wilaya hiyo inatumia megawati saba.

Mhandisi Mlalo alisema kutakuwa na njia tatu za kwenda Urambo,tatu za kwenda wialayani Kaliua ambapo katika kituo cha Urambo- Ipole wilayani Sikonge, ujenzi umefikia asilimia 88 ambapo Mkandarasi kutoka china TBEA anaendelea kufanya kazi nzuri.

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Habari njema
Jambo letu kubwa
lipo kwenye kona...
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com

MAKALA MAALUM

# Itungwe sheria ya kudhibiti ubadhirifu fedha za umma

**Na Ludovick Utouh**

**KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii ya kiuchambuzi, niliainisha mambo saba yanayokwamisha utekelezaji wa hoja za ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), hata kufanya kasoro hizo kuendelea kujirudia.**

**Kuhusu nini kifanyike kufutwa kasoro hizo, kwa kutumia uzoefu wangu, ninapendekeza hatua sita zinazoweza kuwa msaada mkubwa wa kufikisha ukomo wa dosari hizo. Endelea...**



CAG mstaafu Ludovick Utouh.

KUTOKANA na mambo makuu hayo saba niliyoeleza katika toleo la jana lililozama zaidi katika kasoro endelevu zinazojitokeza kwenye utekelezaji hoja za CAG, ninapenda kuhitimisha kuwa, pamoja na dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma, bado kuna maeneo kadhaa yanayohitaji nguvu zaidi kama ifuatavyo:

Moja; Ili kuongeza utekelezaji mapendekezo yanayotolewa katika ripoti za CAG, WAJIBU (taasisi anayoongoza kwa sasa) inashauri Katibu Mkuu Kiongozi kupitia uchambuzi ambao umefanyika, kuwataka watumishi wote ambao wanapaswa kuchukua hatua wajieleze ni hatua gani wamechukua na endapo ikibainika kuwa hawajachukua hatua, basi wachukuliwe hatua wao kwa kushindwa kuchukua hatua.

Ni vyema Katibu Mkuu Kiongozi akafuata mtiririko wa kiutumishi wa kuwajibisha wahusika ili kuimarisha mfumo huo.

Mbili; pamoja na mikakati inayoendelea ya kuboresha mifumo ya ukaguzi wa ndani ikiwamo kuipatia kasma Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani, WAJIBU inaishauri serikali kuboresha mfumo wa utoaji ripoti za utendaji wa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kwa kuitaka idara hiyo kuwasilisha ripoti zake kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kama ilivyo sasa, lakini ripoti hiyo iwasilishwe kwa Katibu Mkuu Kiongozi ili iwasilishwe katika vikao vya Baraza la Mawaziri.

Ikumbukwe kuwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani anakagua mifumo ya usimamizi ya ndani ya serikali yote na si ya Wizara ya Fedha pekee, ndio maana kuna umuhimu wa ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuifikia serikali yote kupitia Baraza la Mawaziri.

Kwa kufanya hivyo, kutaifanya serikali, hasa Rais ambaye ndiye kiranja mkuu wa serikali kujua udhaifu wa utendaji wa mifumo ya ndani ya usimamizi wa fedha za umma na kuchukua hatua mapema kabla ya kutolewa ripoti za CAG.

Tatu; ili kuimarisha mfumo wa sheria na kanuni zinazosimamia ukusanyaji na matumizi ya fedha za umma, WAJIBU inashauri serikali kuja na Sheria ya Ubadhirifu wa Fedha za Umma (Fraud Act) kama zilivyofanya nchi nyingi mbalimbali duniani mwaka 2006.

Kupitia sheria hii, serikali irahisishe utaratibu wa kutambua wahusika wa vitendo vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu pamoja na kuelekeza hatua mahsusi za kuchukua kwa watumishi hao.

Kupitia sheria hii, serikali ipunguze hatua za kiutawala/kinidhamu za kushughulikia vitendo hivi, badala yake iweke hatua za kisheria mahsusi za kushughulikia wahusika wa vitendo hivyo vya ufisadi dhidi ya fedha na rasilimali nyingine za umma.

Sheria kama hii ni sheria mpya iliyobuniwa na nchi mbalimbali kwenye miaka 2000 (hasa 2006) baada ya kupitia adha ya fedha na rasilimali nyingine za umma kurubuniwa na watu wasio waaminifu katika utumishi wao serikalini. Sheria hii hivi sasa inatumika katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Uingereza, Marekani na Kenya.

Nne; ili kuongeza kasi ya kupambana na rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika sekta ya umma, WAJIBU inashauri serikali kuitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuharakisha uchambuzi wa ripoti za CAG ili kubaini maeneo yenye rushwa, udanganyifu na ubadhirifu wa rasilimali za taifa ili wawafikishe kwenye vyombo vya sheria watumishi wote waliohusishwa na vitendo hivyo.

WAJIBU pia inashauri ripoti ya mwaka ya utendaji kazi wa TAKUKURU inayowasilishwa kwa Rais sambamba na ripoti za CAG kila mwishoni wa mwezi Machi, iwasilishwe bungeni kama ripoti za CAG zinavyowasilishwa na baadaye kufanywa wazi kwa umma.

Kuifanya ripoti hii kuwa wazi kwa umma kutawezesha wananchi kuwa na uelewa wa juhudi zinazofanywa na serikali kupitia TAKUKURU katika kupiga vita na kuzuia vitendo vya rushwa nchini, hivyo kupanua nafasi ya ushiriki wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa.

Kufanya hivi pia kutaongeza imani ya wananchi kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na vitendo vya rushwa nchini.

Tano; ili kuboresha utendaji wa mashirika na taasisi za umma, WAJIBU inashauri pamoja na mambo mengine, viongozi wa mashirika na taasisi hizo wapatikane kwa njia ya kiushindani kwa kuzingatia weledi wao katika sekta husika ya shirika/taasisi hizo na malengo mahsusi ya shirika/taasisi hizo.

Viongozi watakaopatikana kwa njia za kiushindani wawekewe malengo ya kiutendaji kwa kuzingatia faida inayotarajiwa pamoja na malengo mengine mahsusi ya kuanzishwa kwa shirika au taasisi husika.

Vilevile, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha mashirika yaliyoanzishwa kwa malengo ya kufanya biashara kwa madhumuni ya kutengeneza faida na kulipa gawio serikalini, yapewe mitaji ya kutosha ya uendeshaji kibiashara.

Jitihada zote zinazofanywa hivi sasa na Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina za kuyapanga upya mashirika ya umma nchini (restructuring) zinapaswa kuungwa mkono na wananchi wote pamoja na wadau wa maendeleo ya nchi yetu.

Sita; Serikali iendelee kutilia mkazo utekelezaji Mpango Mkakati wa Kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP - VI) pamoja na kuongeza kasi ya uundwaji mifumo ya kielektroniki kwa kutumia wataalamu wazawa.

Vilevile, serikali iongeze juhudi za kuvutia sekta binafsi hasa wafanyabiashara na taasisi za kiraia katika kuchangia kwenye uboreshaji mifumo ya usimamizi wa fedha za umma.

Watanzania tuna kila sababu ya kusubiri kwa shauku kubwa ujio wa ripoti za CAG za mwaka 2022/23 ambazo zinatarajiwa kukabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwezi huu wa Machi 2024 na baadaye kuwasilishwa bungeni mwezi Aprili 2024.

Serikali na Bunge zitakuwa zimefanya kazi zake za usimamizi wa utekelezaji mapendekezo ya CAG kama ilivyokuwa inahimizwa na Mheshimiwa Rais na viongozi wengine wakuu wa serikali, tutarajie kuwapo uboreshwaji katika hoja za ukaguzi katika ripoti za mwaka huu kulinganishwa na miaka iliyopita.

Vinginevyo, kama hali itakuwa mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka jana, basi serikali ione umuhimu wa kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa hapo juu na Taasisi ya WAJIBU - Institute of Public Accountability.

***Mwandishi wa makala hii ya kiuchambuzi ni CAG mstaafu, pia alishakuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na Mhadhiri wa Uhasibu Chuo Kikuu cha Mzumbe.**

# Deni la bil.7/- lakwamisha ukamilishaji ujenzi wa vivuko

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeiagiza serikali kumlipa mkandarasi Songoro Marine Transport Ltd Sh.bilioni saba anazodai ili akamilishe ujenzi wa vivuko.

Akizungumza juzi baada ya kamati hiyo kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa mkandarasi huyo, Mwenyekiti kamati hiyo, Selemani Kakoso alisema wananchi wengi wa Kanda ya Ziwa wanauhitaji wa vivuko hivyo.

Hivyo, aliamuagiza Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa kuhakikisha anapeleka fedha hizo kwenye huo mradi ili uweze kukamilishwa kwa wakati na kutowarudisha nyuma makandarasi wazawa katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Hapa angekuwa mkandarasi kutoka nje ya nchi lazima mgemlipa riba lakini kwa kuwa ni mkandarasi mzawa bado na yeye anahitaji kuendelea kukua ataishi kwa maumivu makali anaogopa akiwadai kwa kulazimisha mtamnyima tenda, ndicho kinachowaua wazawa" alisema Kakoso.

Baada ya maagizo hayo, Waziri Bashungwa aliahidi kufuatilia suala hilo baada ya ziara hiyo ambapo alisema ataenda kuweka kambi hazina kwa ajili ya kumuomba Waziri wa Fedha na wataalamu wake kulizingatia hitaji kubwa la mkandarasi huyo kulipwa fedha hizo ili wananchi waweze kupata huduma baada ya miradi hiyo kukamilika.

Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa kivuko kipya na maegesho ya Buyagu- Mbalika alisema kivuko hicho chenye urefu wa mita 30.25, upana mita 9.75 kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 50, abiria 100 na magari madogo sita.

Alisema mpaka sasa mradi huo umefikia asilimia 45.9 na umeongezwa muda kwa miezi minne bila ongezeko la gharama kutokana na kuchelewa kwa malipo baada ya kuwasilisha hati za madai.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Songoro Marine Transport, Meja Songoro alisema tatizo walilokutana nalo ni kuchelewa kwa malipo ambapo mpaka sasa ni zaidi ya Sh.bilioni Saba.

"Katika karakana yetu ya Mwanza tunatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo Rugezi - Kisorya ambao umefikia asilimia 81, Ijinga -Kahangala asilimia 84, Bwiro - Bukondo asilimia 85, Nyakalilo- Kome asilimia 60 na Buyagu - Mbalika asilimia 45.9" alisema Songoro.

## HABARI KITAIFA




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Diamond Trust (DTB), Ravneet Chowdhury (kushoto), akikabidhi msaada wa kompyuta 100 zenye thamani ya Sh. milioni 35 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Kuendeleza Elimu cha Lauren (LEPC), Felicia Felix (wa pili kushoto), Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Songoro Mnyonge, Ronadina Kimaro (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha msaada kwa Wajane na Watoto (CWCA), Utti Mwang'amba, zilizotolewa na benki hiyo, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam jana, ikiwa ni mkakati wake wa ushirikiano na jamii wa kuendeleza elimu ya TEHAMA kwenye shule za sekondari. **PICHA: MARY KADOKE**

# Wabunge Uganda wajifunza TCRA inavyosimamia mawasiliano nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Bunge ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Miongozo ya Kitaifa kutoka Uganda, ikishirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano ya Uganda (NITA-U), imetembelea Ofisi Kuu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Lengo la ziara ni kujifunza Tanzania inavyosimamia sekta ya mawasiliano, ikihusisha mawasiliano ya simu, intaneti, utangazaji na huduma za posta.

Ujumbe huo uliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Tony Ayoo, wajumbe wakipata fursa ya kuelewa TCRA inavyohudumia wadau mbalimbali katika sekta ya mawasiliano, ikiwamo wamiliki wa leseni, watumiaji huduma za mawasiliano na wadau wa sekta ya umma.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, John Daffa, akizungumza na ugeni huo, alisema: "Jukumu letu ni kuhakikisha kwamba huduma zote zinazohusu mawasiliano, zilizo ndani ya ikolojia ya teknolojia ya habari na mawasiliano zinasimamiwa kwa ufanisi ili zichangie maendeleo ya nchi.

Kamati hiyo pia ilijifunza kuhusu TCRA inavyotekeleza majukumu yake ya kusimamia rasilimali muhimu za mawasiliano kama vile masafa ya mawasiliano, nambari za mawasiliano, kikoa cha taifa cha tz, kanzidata ya anwani na postikodi.

Vilevile, alisema walijifunza kuhusu uboreshaji utoaji leseni za mawasiliano, ambazo sasa zinapatikana kwa njia ya mtandao kupitia jukwaa la Tanzanite, hivyo kuondoa ulazima wa waombaji kufika ofisini.

"Tumeweka mfumo wa utoaji leseni mtandaoni, unaorahisisha upatikanaji leseni kwa waombaji wapya na kupunguza changamoto za ufuatiliaji leseni kwa wawekezaji, maboresho haya yameleta ufanisi mkubwa katika usimamizi wa mawasiliano nchini," alifafanua.

Kuhusu upatikanaji teknolojia ya mawasiliano, Daffa alisema TCRA inahakikisha wananchi wanapata huduma za mawasiliano ya kasi na zenye ubora.

Alitaja upatikanaji teknolojia ya mawasiliano ya simu kufikia asilimia 98 kwa 2G, asilimia 86 kwa 3G, asilimia 79 kwa 4G, na asilimia 10 kwa teknolojia ya 5G.

Aidha, wajumbe hao walijifunza kuhusu usimamizi wa masafa ya utangazaji wa redio, usimamizi wa kikoa cha taifa cha .tz, utangazaji wa redio kidijitali na jinsi Tanzania inavyowezesha vijana kushiriki katika uchumi wa kidijitali.

Akijibu hoja za wabunge hao, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Daffa alisema TCRA imeanzisha mfumo wa kiusimamizi unaoimarisha usimamizi wa sekta za simu, intaneti, utangazaji na posta.

Kuhusu utangazaji wa redio kidijitali, alibainisha kuwa TCRA inaandaa mwongozo utakaowezesha Tanzania kuanza kutumia teknolojia ya Digital Sound Broadcasting.

# TGNP yaibua hoja bajeti jumuishi makundi yote

**Na Zanura Mollel**

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) umependekeza serikali kuwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 kuwa na mtazamo wa usawa wa kijinsia kwa kuzingatia makundi yote ambayo yanatajwa kuchangia pato la taifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gemma Akilimali, alisema hayo jana katika kikao kazi cha kuchakata mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 kilichoshirikisha wadau mbalimbali wakiwamo watumishi wa serikali za mitaa.

Alisema bajeti ya serikali inalenga mapato na matumizi na kila Mtanzania ana mchango mkubwa katika bajeti hiyo lakini katika matumizi imeonekana wananchi kuachwa nyuma hususani maeneo ya vijijini na mijini.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, uwapo wa bajeti jumuishi yenye mlengo wa kijinsia haimanishi kuzingatia wanawake bali ni bajeti ya matumizi ambayo itagawanywa kwa makundi yote kutokana na mchango wa kila kundi.

Alisema kumekuwapo malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi kwenda kwa viongozi hususani wa halmsahauri kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali na hilo limekuwa likibainika katika ufuatiliaji.

"Halmashauri wakati mwingine zinakuwa hazijaingiziwa fedha ndiyo maana kunakuwa na malalamiko lakini kama zimeingizwa na miradi kutotekelezwa hiyo si sawa," alisema.

Alisema wananchi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kufuatilia fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi katika maeneo yao kwa kuhoji na kulinganisha thamani ya fedha na mradi unaotekelezwa ili kudhibiti mianya ya ubadhirifu.

"Serikali imeanza kuchakata muda wa matumizi kwa wale ambao wameonekana kujishughulisha na kazi za ziada zikiwamo shughuli za nyumbani za kinamama ili nao wanufaike na bajeti ya nchi," alisema.

Hata hivyo, alisema kunufaika kwa bajeti hiyo si kupatiwa fedha bali ni kuhakikisha huduma za kijamii zinasogezwa karibu zikiwamo upatikanaji wa nishati ya umeme, maji safi na salama, miundombinu ya elimu na afya.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema lengo la kukutana na wadau hao ni kuichakata bajeti kwa kuangalia upungufu na kasoro kisha kushauri kufanyiwa maboresho kabla haijapitishwa na bunge.

Alisema mkakati wa maendeleo wa miaka mitano kwa mwaka 2022/23 ulizangatia bajeti jumuishi yenye usawa wa kijinsia kati ya mikakati mitano, mitatu ilizingatia "matokeo haya ni chachu ya mashirika na wadau wanaoshinikiza usawa katika mgawanyo wa fursa hapa chini".

Sophia Komba, kutoka kituo cha kupinga ukatili wa kijinsia Dar es Salaam alisema mafunzo hayo yatabadili mitazamo kwa jamii ikiwamo watendaji wa serikali za mitaa walioshiriki katika semina hiyo kwa kupata uelewa kuwa bajeti ni ya watu wote.

"Ukienda kuomba taarifa ya bajeti huko halmashauri ni vigumu kupatiwa. Wanasema ni taarifa za serikali, hivyo kupitia haya mafunzo watumishi walioshiriki watatambua kuwa kila mtu ana haki ya kujua bajeti inayotekelezwa katika maeneo yao," alisema Komba.


**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TZ)**

## TANGAZO KWA UMMA

### ZOEZI LA UBOMOAJI WA NYUMBA ZILIZOFIDIWA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) alianza kuwalipa fidia waathirika wa mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kuanzia mwezi Novemba 2023. Kwa mujibu wa makubaliano ya ulipaji wa fidia, waathirika wanatakiwa kupisha eneo la mradi ndani ya wiki sita (6) baada kupokea fedha kwenye akaunti zao. Muda huu umeshakamilika kwa idadi kubwa ya waathirika.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa kushirikiana na ofisi za Wakurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni, inatarajia kuendesha zoezi la ubomoaji wa nyumba zilizofidiwa kuanzia tarehe 12/04/2024. Hivyo waathirika wa mradi wanatakiwa kupisha eneo la mradi kabla ya tarehe tajwa hapo juu. Ikumbukwe kuwa ubomoaji huu unawahusu waathirika wa mradi ambao wameshapokea fidia katika akaunti zao kwa muda usiopungua wiki sita (6) tangu siku ya kuanza zoezi hili.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hatua stahiki zichukuliwe katika kukabiliana na vitendo hivi viovu

**TANZANIA** imekuwa ikichukua tahadhari mbalimbali dhidi ya matishio yanayoweza kujitokeza yakiwamo ya ugaidi hasa kutokana na kuwapo kwa vikundi vinavyojihusisha na vitendo hivyo katika nchi jirani. Miongoni mwa hatua hizo ni kutungwa kwa Sheria ya Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2022 ambayo msukumo mkubwa ulitokana hasa na uvamizi wa ofisi za ubalozi Dar es Salaam na Nairobi, Kenya mwaka 1998.

Aidha, katika kupambana na vitendo hivyo kwa kuzingatia kuwa inapakana na mataifa mbalimbali, Tanzania kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, imekuwa ikiweka ulinzi wa kutoka kwenye maeneo ya mipaka. Lengo ni kuhakikisha viashiria vya vitendo vyovyote vya kigaidi pamoja na uingiaji wa wahamiaji haramu vinadhibitiwa na kukomeshwa.

Pamoja na kujizatiti huko, taarifa iliyotolewa karibuni inaonyesha kuwa Tanzania haina mifumo mizuri ya usimamizi na ufuatiliaji wa mienendo wa jumuiya za kiraia zikiwamo taasisi na madhehebu ya dini. Hali hiyo inasababisha kuwapo kwa hatari ya taasisi hizo hasa madhehebu ya dini kutumika katika utakatishaji fedha haramu au kufadhili masuala ya kigaidi.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamadi Masauni, alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni za usajili wa jumuiya huku akiweka bayana kwamba baadhi ya jumuiya za kiraia zimeripotiwa kujihusisha au kutumika katika kufanikisha kutendeka kwa makosa ya jinai na vitendo vingine vyenye madhara kwa jamii.

Miongoni mwa makosa hayo, kwa mujibu wa Waziri Masauni ni utakatishaji wa fedha haramu, ugaidi na ufadhili wa shughuli za kigaidi, usafirishaji haramu wa binadamu, biashara haramu ya silaha na uwapo wa jumuiya za kidini zinazotoa mafundisho potofu na hatarishi kwa usalama wa raia (afya ya mwili na akili).

Kutokana na kuwapo kwa taasisi hizo, alisema hali hiyo imesababisha Tanzania kuwekwa katika kundi la nchi zinazohitaji ufuatiliaji wa karibu. Pia hali hiyo inaharibu taswira nzuri ya Tanzania katika medani ya diplomasia ya kimataifa iliyopo sasa.

Kuna msemo kwamba ukiona panafuka moshi ujue pana moto au unapodhania pana amani, uharibifu upo. Taarifa hiyo inabainisha kwamba Tanzania si nchi salama kwa kiwango cha juu kama inavyoaminika bali kuna viashiria vya kuwapo matendo maovu yakiwamo ya kigaidi. Kwa mantiki hiyo, taarifa hiyo inatuamsha kutoka usingizini kwamba tunapaswa kuamka na kuchukua tahadhari.

Ni kweli kwamba hivi sasa kumeibuka madhehebu mengi ya dini hata katika maeneo ya makazi na wengine wanafanya ibada katika vituo vya mabasi. Jambo la kujiuliza je, mafundisho yanayotolewa na wahubiri hao yanafuata misingi ya mafundisho halisi ya dunia husika?


Jambo lingine la kujiuliza ni kama kuna ufuatiliaji wa kutosha kujua matendo na mienendo ya taasisi hizo. Tunasema hivyo kwa kuwa kuna uwezekano wa kuwapo viashiria vya utakatishaji fedha na mipango ya chini kwa chini kutokana na kufadhiliwa na watu ambao huenda hawana nia njema na usalama wa nchi.

Kama alivyosema Waziri, ni dhahiri kwamba kuna udhaifu katika ufuatiliaji ndiyo maana ripoti inaonyesha kwamba kuna tatizo kubwa katika eneo hilo. Kwa mantiki hiyo, ni vyema kikaundwa kitengo cha tathmini na ufuatiliaji ili kubaini mienendo ya uendeshaji wa taasisi hizo.

Wakati wa serikali ya awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, baadhi ya viongozi wa dini walituhumiwa kujihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya. Jambo hilo pia lichukuliwe kwa uzito kama rejea na kuanza kufanyia kazi viashiria vya vitendo viovu vilivyoainishwa kwenye ripoti.

Hali hiyo inatokana na ukweli pia kwamba baadhi ya viongozi wa madhehebu hayo badala ya kuwahubiria watu masuala ya imani, ikiwamo kutenda matendo mema na kuishi maisha yasiyo na uchochezi, wamekuwa wanafundisha masuala ya utajirisho. Ni vyema hatua zikaanza kuchukuliwa sasa kabla mambo hayajafikia hatua mbaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Magonjwa yasiyoambukizwa yalivyo hatari na gharama ya kimyakimya

Na Adam Fungamwango

**KUNA** ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukizwa nchini Tanzania kwa miaka ya hivi karibuni.

Jopo la madaktari bingwa wa magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya Moyo, Jakaya Kikwete (JKCI), limefanya uchunguzi pamoja na kutoa huduma kwa wagonjwa 10,807 kutoka mikoa 13 nchini na kubaini shinikizo la damu ni tatizo kubwa nchini.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni mkoani Kagera na Daktari Bingwa wa Moyo na Mfumo wa Umeme wa Moyo, Yona Gaudiye.

Akasema kuwa kati ya hiyo, wagonjwa 194 wanahitaji huduma zaidi ya kuchunguza, upande wa magonjwa hayo ya moyo.

Sababu zinazosababisha ugonjwa na moyo, pamoja na magonjwa mengine yasiyo ya kuambukiza ni zile zile.

Alizitaja kuwa ni ulaji usio sahihi, mtindo wa maisha, matumizi ya sigara, unene uliopitiliza, unywaji wa pombe uliokithiri, upungufu wa madini ya potassium na magonjwa sugu ya figo.

Binafsi niseme tu kuwa, ongezeko kubwa la magonjwa hayo yalianza kujitokeza kwa wiki mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Na hii ilitokana na aina ya maisha ya wakati huo ambayo pamoja na kwamba yalionekana si ya kisasa, lakini yalichangia mno kuepukana na magonjwa hayo.

Wengi walikuwa wanakwenda kazini na mabasi ya abiria, na baadhi kwa miguu. Ni wachache sana walikuwa na magari binafsi.

Hata wanafunzi walitembea umbali mrefu kwenda shuleni, wale wa vijijini ndiyo kabisa walitumia kilometa kadhaa kabla ya kufika shuleni na kurejea nyumbani.

Hakukuwa na mabasi ya shule kama hivi sasa ambayo pamoja na malezi ya 'kimayai' yanasababisha watoto wawe na unene uliopitiliza na kuanzisha tatizo bado mapema kabisa.

Kipindi hicho hakukuwa na usafiri wa bajaji, au bodaboda ambao, pamoja na kupunguza tatizo la usafiri, lakini nyuma ya pazia ni moja ya vitu vilivyoongeza magonjwa yaliyoambukizwa, hususan moyo, kwani umbali hata wa kilometa moja tu, mtu anachukua usafiri huo badala ya kutembea kwa miguu ili kuupa mazoezi mwili.

Nasema hivi, kwa sababu katika miaka ya 1960, 1970, 1980 hadi 1990, magonjwa kama ya moyo, kisukari, kupooza ilionekana ni ya matajiri zaidi na si ya watu masikini.

Ni kweli, kwa sababu wagonjwa walioonekana nayo ni wale wanaojiweza. Ni kwa sababu wao waliishi maisha ya fahari, anasa, wakila wanachokitaka, hasa vyakula vya mafuta, vinavyooakisi uwezo wao, na mazoezi kwao ilionekana kama kujisumbua tu.

Waliokuwa na kipato cha chini hawakuugua siyo kutokana na kitu chochote kile, ila wao walikuwa wakihenyeka, hivyo kufanya mazoezi bila wao kujua, na hata kula walikula vyakula vya kawaida ambayo wao waliona ni vya kimasikini, lakini kiafya ndiyo vilitakiwa wale. Siku hizi wengi wana magari. Mtu anashinda ofisini amekaa, anatoka anaingia kwenye gari, ana kwenda nyumbani anapumzika, analala, kesho anaingia kwenye gari lake kuwahi kazini.

Huo unakuwa ndiyo mtindo wa maisha yake, huku akila vyakula vyenye mafuta ambavyo havisumbuliwi na mazoezi yoyote mwilini. Ni lazima magonjwa kama haya waongezeke.

Binafsi nawashauri Watanzania kuwa makini sana na ulaji pamoja na mtindo wa maisha. Siku zote vyakula vyenyewe vyenye afya ni rahisi sana sokoni na dukani, kuliko vile vitamu, vya kifahari vinavyoleta magonjwa.

Tuwe na tabia ya kujitesa. Kufanya mazoezi na kuusumbua mwili. Kufunga mara kwa mara na kupenda kutembea kwa umbali mrefu angalau mara moja moja.

Nasema hivi kwa sababu gharama za magonjwa yasiyoambukizwa ni kubwa mno, ambapo wenye kipato kidogo itamuwia ngumu yeye na familia yake kumudu.

Waswahili wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta, Watanzania wanapaswa sasa waanze kuepuka maisha ya 'ubosi' ili kuepukana na hayo, kwani hata wale mabosi wenyewe halisi wa kisasa wameshajua hilo, na wamekuwa wakifanya mazoezi kiasi kwamba hata ukiwaona hutoamini kama ni wao. Sasa kama wao wenye uwezo wa kipesa na mamilionea wanaogopa magonjwa hayo, sembuse raia wa kawaida tu?

Afya ndiyo mtaji namba moja wa binadamu ambao hauna mbadala wake, tujitunze kwa kufanya mazoezi, kula mlo kamili kwa kiasi na kuepuka vyakula vinono, vyenye mafuta mengi na vyenye ladha tamu mdomoni ambayo vingi huwa na athari kwa afya zetu.

# Wabunge Uganda wajifunza TCRA inavyosimamia mawasiliano nchini

Na Mwandishi Wetu

KAMATI ya Bunge ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Miongozo ya Kitaifa kutoka Uganda, ikishirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano ya Uganda (NITA-U), imetembelea Ofisi Kuu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Lengo la ziara hiyo lilikuwa kujifunza jinsi Tanzania inavyosimamia sekta ya mawasiliano, ikihusisha mawasiliano ya simu, intaneti, utangazaji, na huduma za posta.

Ujumbe huo uliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Tony Ayoo, kisha wajumbe walipata fursa ya kuelewa TCRA inavyohudumia wadau mbalimbali katika sekta ya mawasiliano, ikiwemo wamiliki wa leseni, watumiaji wa huduma za mawasiliano, na wadau wa sekta ya umma.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, John Daffa, akizungumza na ugeni huo, alisema: "Jukumu letu ni kuhakikisha kwamba huduma zote zinazohusu mawasiliano, zilizo ndani ya ikolojia ya teknolojia ya habari na mawasiliano, zinasimamiwa kwa ufanisi ili zichangie maendeleo ya nchi yetu. Kamati hiyo pia ilijifunza kuhusu namna TCRA inavyotekeleza majukumu yake ya kusimamia rasilimali muhimu za mawasiliano kama vile masafa ya mawasiliano, nambari za mawasiliano, kikoa cha taifa cha .tz, kanzidata ya anwani na postikodi.

Vilevile, alisema walijifunza kuhusu uboreshaji wa utoaji wa leseni za mawasiliano, ambazo sasa zinapatikana kwa njia ya mtandao kupitia jukwaa la Tanzanite, hivyo kuondoa ulazima wa waombaji kufika ofisini.

"Tumeweka mfumo wa utoaji leseni mtandaoni, unaorahisisha upatikanaji wa leseni kwa waombaji wapya na kupunguza changamoto za ufuatiliaji wa leseni kwa wawekezaji, maboresho haya yameleta ufanisi mkubwa katika usimamizi wa mawasiliano hapa nchini," alifafanua. Kuhusu upatikanaji wa teknolojia ya mawasiliano, Daffa alifafanua kwamba TCRA inahakikisha wananchi wanapata huduma za mawasiliano ya kasi na zenye ubora.

Alitaja upatikanaji wa teknolojia ya mawasiliano ya simu kufikia asilimia 98 kwa 2G, asilimia 86 kwa 3G, asilimia 79 kwa 4G, na asilimia 10 kwa teknolojia ya 5G.

Aidha, wajumbe hao walijifunza kuhusu usimamizi wa masafa ya utangazaji wa redio, usimamizi wa kikoa cha taifa cha .tz, utangazaji wa redio kidijitali, na jinsi Tanzania inavyowezesha vijana kushiriki katika uchumi wa kidijitali.

# Afya ya mama, mtoto yapokea vifaa mil. 38/-

Na Joseph Mwendapole

MRADI wa USAID Afya Yangu unaotekelezwa na Shirika la Jhepiego, umetoa msaada wa vifaa tiba kwa ajili ya kuboresha afya ya mama na mtoto mkoa wa Dar es Salaam, vyenye thamani ya Sh. milioni 38 .

Msaada huo ulikabidhiwa jana jijini kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Jhpiego, Dk. Mteule Amon.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Dk. Amon alisema ni matumaini ya Jhpiego kwamba msaada huo utapunguza changamoto ambazo mama na mtoto wamekuwa wakizipata kwa mkoa mzima wa Dar es Salaam.

Alisema mradi wa USAID Afya Yangu, unafadhiliwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) Tanzania na ulizinduliwa rasmi kitaifa Juni, 2022 ambao ni wa miaka mitano (2022-2027) ukitekelezwa na Jhpiego Tanzania na washirika wake katika mikoa 11 Tanzania Bara na visiwani, Dar es Salaam ikiwamo.

"Kipekee nikupongeze wewe kwa uongozi wako imara, dhamira na maono yako ambayo yamekuwa dira katika kushughulikia kero za wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Naomba pia nishukuru timu za usimamizi wa afya za Halmashauri na Mkoa ambazo zimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha mradi unatekelezwa kama ulivyopangwa," alisema.

Katika miaka miwili ya utekelezaji, kwa kushirikiana na serikali ngazi zote, alisema mradi umetekeleza afua mbalimbali zinazolenga kuzuia na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto chini ya miaka mitano ikiwamo kuimarisha huduma za uzazi wa mpango. Watoa huduma 97 walipata mafunzo na wateja 27,683 walipata huduma za uzazi wa mpango kupitia huduma za mkoba zilizofadhiliwa na mradi.

Alisema wamefanikiwa kuimarisha huduma za dharura wakati wa kujifungua ambapo watoa huduma 26 wa usingizi wa ganzi, madaktari wanaofanya upasuaji na wauguzi wa vyumba vya upasuaji 39 katika halmashauri za Kigamboni na Temeke walipatiwa mafunzo kazini.

Alisema mradi umetoa mafunzo wezeshi kwenye huduma ya mama na mtoto kwa watumishi 26 ambao waliweza kuwafundisha watumishi wenzao wapatao 214 kutoka katika vituo 127.

Dk. Amon alisema mradi pia umeboresha huduma za chanjo - kusambaza chanjo kutoka katika wilaya kwenda vituo mbalimbali, kuwezesha timu za mkoa/halmashauri kufanya usimamizi shirikishi na kuwezesha vituo 165 kutoa huduma za chanjo katika ngazi ya jamii.

Alisema walitoa mafunzo ya lishe kwa watoa huduma wezeshi 39 na mafunzo hayo yamewezesha watoa huduma hao kuwajengea uwezo watoa huduma wengine wapatao 424 kwenye vituo vyao kuweza kuchunguza, kugundua na kutibu utapiamlo mkali kwa kutumia chakula dawa itokanayo na vyakula vya asili.

Chalamila alipongeza shirika hilo kwa msaada huo ambao alisema utakwenda kuwa msaada mkubwa kwa mama na mtoto kwenye mkoa huo na kuwataka wahusika kuhakikisha msaada huo unatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuwanufaisha walengwa.

Alisema serikali inathamini michango ya wadau mbalimbali ambao wanaendelea kushirikiana katika kuboresha afya kwa watanzania kwa ujumla akisema kuwa afya ni jambo la msingi ambalo serikali imelipa kipaumbele.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA ULIOKAGULIWA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2023 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2022 |
|---|---|---|---|
| A | **ASSETS** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 511.52 | 595.79 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 9,797.16 | 4,942.86 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 38,180.41 | 43,769.98 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,117.74 | 504.40 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22.94 | 0.04 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 3,517.44 | 4,179.14 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 46,709.06 | 50,045.18 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,523.75 | 1,347.58 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | 14 Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 824.19 | 1,149.36 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **102,204.21** | **106,534.34** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,700.00 | 9,984.60 |
| | 18 Amana za Wateja | 56,378.31 | 53,334.13 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| | 20 Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0.00 | 0.00 |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,101.03 | 1,652.44 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| | 27 Dhima Nyingine | 717.28 | 921.31 |
| | 28 Madeni | 0.00 | 0.00 |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **60,896.62** | **65,892.48** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **41,307.59** | **40,641.86** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 261.30 | 467.69 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 7,386.41 | 6,448.73 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 829.89 | 895.43 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 0.00 | 0.00 |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0.00 | 0.00 |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,307.59** | **40,641.86** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 4,446.26 | 6,747.30 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 349.31 | 2,181.49 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 178.13 | 80.66 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 40.42% | 38.15% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.74% | 4.35% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80.69% | 79.15% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 45.70% | 46.98% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87.66% | 92.46% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | -8.28% | -31.98% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | -4.06% | -21.27% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2023 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2022 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 8,529.50 | 8,707.52 |
| 2 Gharama za Riba | 2,985.09 | 3,258.97 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,544.41** | **5,448.54** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 100.09 | 6.13 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 258.71 | 951.18 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **646.84** | **703.93** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 122.86 | 196.93 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 523.98 | 507.00 |
| 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0.00 | 0.00 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **4,208.26** | **3,839.70** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 1,570.03 | 1,633.82 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 28.59 | 34.07 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 2,609.64 | 2,171.82 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,624.19** | **1,355.47** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 794.30 | 460.03 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **829.89** | **895.43** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 26 | 26 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 25 | 27 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 25 | 27 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.79% | 0.76% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.02% | 2.19% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 67.97% | 62.41% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.90% | 5.04% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 Desemba 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2023 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2022 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 829.89 | 895.43 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | 0.00 | 0.00 |
| | Hasara katika mali | 778.63 | 1,371.25 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | 3,272.45 | 95.22 |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | 0.00 | 0.63 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | (5,240.42) | (29,765.88) |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 456.91 | 193.30 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 312.96 | 807.91 |
| | Kodi iliyolipwa | (694.80) | (700.82) |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(284.37)** | **(27,102.95)** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (417.76) | (148.55) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 0.00 | 9.03 |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (7.93) | (7,000.05) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(425.69)** | **(7,139.57)** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | (164.15) | (492.45) |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(Malipo ya dhima kukodishwa)-IFRS 16 | (253.88) | (280.53) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(418.03)** | **(772.98)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(1,128.10)** | **(35,015.50)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa mwaka | 12,085.80 | 47,101.30 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa mwaka** | **10,957.71** | **12,085.80** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI ILIYOKAGULIWA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2023** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 7,344.16 | 467.69 | - | - | **40,641.86** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 829.89 | - | - | - | **829.89** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (164.15) | - | - | - | **(164.15)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 206.39 | (206.39) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | - | **8,216.29** | **261.30** | - | - | **41,307.59** |
| **Mwaka Uliopita 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 6,129.50 | 1,279.37 | - | - | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 895.43 | - | - | - | **895.43** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 811.68 | (811.68) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | - | **7,344.16** | **467.69** | - | - | **40,641.86** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2023

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | MKURUGENZI MKUU | (IMESAINIWA) | 20-03-2024 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (IMESAINIWA) | 20-03-2024 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (IMESAINIWA) | 20-03-2024 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 20-03-2024 |
| MWANAIDI A MTANDA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 20-03-2024 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kulia), akiagana na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Fedha NMB, Juma Kimori.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu aagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa zijifunze NMB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imefuturisha wateja wake walio kwenye Mfungo wa Mwezi wa Ramadhani jijini Dar es Salaam, huku ikitoa misaada kwa vituo vya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameguswa na msaada huo na kuagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi za fedha zijifunze kwa NMB namna ya kuthamini wenye uhitaji.

Hafla hiyo ya Iftar ilifanyika juzi jijini Dar es Salaam, ikiwa ni ya tatu kuandaliwa na Benki ya NMB tangu kuanza kwa ibada ya Funga ya Ramadhani ambayo ni Nguzo ya Pili kati ya tano za Dini ya Kiislamu.

Hafla zingine zilizoandaliwa na benki hiyo zimefanyika katika Visiwa vya Unguja na Pemba, ambako pia kulitolewa misaada ya kijamii kwa watoto wenye uhitaji.

Waziri Mkuu Majaliwa alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyohudhuriwa na zaidi ya watu 1,200, wakiwamo wateja wa NMB, wadau, viongozi wa serikali, watoto wanaoishi katika mazingira magumu wa vituo vya Al-zam (Mbagala), Umrah (Magomeni Mikumi) na Tanzania Kwanza (Tuangoma, Kigamboni).

Akizungumza mbele ya waalikwa hao, Waziri Mkuu Majaliwa alisema NMB inastahili pongezi kwa namna inavyoyajali makundi mbalimbali ya kijamii, ikiwamo kuunga mkono sapoti jitihada za elimu katika sekta za elimu, afya, maji, michezo na elimu za fedha kwa wajasiriamali.

"Leo hii (juzi) nitapokea kutoka kwa NMB zawadi maalum kwa ajili ya watoto wenye uhitaji wa vituo vya Al-zam, Umrah na Tanzania Kwanza vya Dar es Salaam. Kwa hili NMB mmefanya jambo kubwa sana, mnataka watoto hawa wajione kuwa wana thamani sawa na wengine.

"Ninatambua kuwa licha ya kukumbuka watoto wenye uhitaji, mmekuwa pia mkichangia mahitaji kwenye shule zinazotumiwa na watoto wenye mahitaji maalum.

"NMB pia ni benki inayoongoza kwa utoaji huduma nchini kwa sasa, imetenga Sh. trilioni moja kwa ajili ya kuhudumia sekta ya kilimo nchini, hii ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anakamilisha miaka mitatu ya uongozi wake madarakani," alisema.

Waziri Mkuu alisema NMB ni benki ya ubia, na serikali ikiwa na hisa na ni mnufaika wa hisa ilizonazo. Alitoa mfano wa gawio kubwa, rekodi ikiwekwa mwaka 2023, benki hiyo ilipotoa gawio la Sh. bilioni 45.3 kwa serikali, kiasi ambacho hakijawahi kutolewa na mbia yeyote wa serikali kama gawio.

Alitumia nafasi hiyo kupongeza vituo vya watoto yatima na watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kimaendeleo katika umri wao, na kwamba NMB inaongoza njia inayopaswa kupitwa na taasisi nyingine kiasi cha kutaka ziige mwenendo huo.

"Kama ambavyo nimetoa wito kwa taasisi na wadau wengine kuiga kwa NMB, Nitumie fursa hii pia kuziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo ni taasisi ya serikali, wastahiki mameya mpo hapa, wakuu wa wilaya mpo hapa, madiwani wachache wawakilishi mpo hapa, lichukueni hili kama ajenda.

"Hakikisheni watoto hawa wenye ulemavu, yatima, wanaoishi mazingira magumu na wenye mahitaji maalum, wasiwe wanafikiwa tu kipindi cha Ramadhani, iwe ni utaratibu wa kila siku katika maisha yao yote. Halmashauri ziratibu mwenendo wao, mahitaji yao, huduma zao, ili watoto hawa tuwalee.

"Hawa ndio Watanzania ambao baadaye watakuwa viongozi wa taifa hili. Kwahiyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa jifunzeni kutoka kwa NMB namna ya kushiriki kikamilifu kutambua vituo na kuvihudumia," aliagiza.

Mbali na Waziri Mkuu Majaliwa, hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila na Meya wa Dar es Salaam, Omar Kumbilamoto.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori, kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, alitoa salamu za shukrani kwa Waziri Mkuu kwa kuhudhuria hafla hiyo, akiwashukuru pia wateja, wadau na viongozi wote waliotikia mwaliko wa taasisi yake kujumuika pamoja.

"Katika kila Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tumekuwa na utamaduni huu wa kupata futari ya pamoja na wateja wetu, wadau, viongozi na waalikwa wengine kama ishara ya upendo, umoja, mshikamano. Ujio wenu ninyi nyote unathibitisha kuwa ninyi ni familia ya NMB.

"Pamoja na futari hii, lakini mwaka huu tutakabidhi misaada kwa watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu. Tuna vituo vitatu hapa vyenye watoto takribani 200, ambavyo tunakwenda kuvipa zawadi za mfungo ili wakitoka hapa waendelee kufurahia Mwezi wa Ramadhani na Sikukuu ya Idd," alisema Kimori.

Awali akimkaribisha Waziri Mkuu, Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema umuhimu wa majumuiko ya namna hiyo ni kujenga jamii ya watu wenye hofu ya Mungu, ambao aliwataja wanahitajika sana katika kukuza uchumi wa nchi na ustawi wa taasisi kama NMB.

"Ofisa Mkuu wa Fedha tayari ameshazungumza kwa kina, kwamba pamoja na ibada ya futari, NMB inakwenda kuwashika mkono wahitaji ambao tumeambatana nao hapa.

"Wito wetu kwa jamii ni kuendelea 'kubenkika' na NMB inayotumia kaulimbiu ya 'Karibu Yako', ili kutanua familia hii," alisema Dk. Mhede.

---

MIAKA 3 YA SAMIA

## JKCI yatoa huduma kwa watu 362,000

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imesema kwa miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, imetoa huduma kwa watu 361,894.

Vilevile, imebainisha kuwa kati ya watu hao, 238,850 (asilimia 66) walikuwa na tatizo la shinikizo la juu la damu.

Pia imebainisha kuwa asilimia 25 ya vifo vitokanavyo na magonjwa ya moyo vinavyotokea duniani, vinasababishwa na ugonjwa wa shinikizo la juu la damu huku ugonjwa huo ukiwa unaongoza kwa kuua watu wengi zaidi.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika taasisi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Samia Suluhu Hassan.

Dk. Kisenge ambaye pia ni daktari bingwa wa magonjwa ya moyo, alisema asilimia 90 ya wagonjwa wa shinikizo la juu la damu hawana dalalili mpaka wapime, wagonjwa wachache wanakuwa na dalili za maumivu ya kichwa, macho kuona kiza, maumivu ya misuli ya shingo, kutoka damu puani na wakati mwingine kupoteza fahamu, maumivu makali kifuani, kizunguzungu na mapigo ya moyo kwenda kas.

"Unapoona dalili hizi wahi hospitalini mapema kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na kupata matibabu, pia ninawasihi watu wajenge tabia ya kupima shinikizo la damu na kiwango cha sukari kwenye damu mara kwa mara na kwa wale watakaokutwa na tatizo na kuanzishiwa dawa, wasiache kuzitumia hata kama watapata nafuu," alisema Dk. Kisenge.

Mtaalamu huyo wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu alisema mtu anaweza kupunguza shinikizo la juu la damu kwa kufanya mazoezi, kuzingatia lishe bora kwa kula matunda, mboga za majani, vyakula vyenye madini ya potassium na kupunguza kula vyakula vyenye kiasi kikubwa cha mafuta na chumvi.

Alisema pia kuna umuhimu kwa watu kuepuka uvutaji wa sigara na unywaji pombe uliokithiri, kutambua kiwango cha sukari mwilini, kutambua msukumo wa damu na kiwango cha mafuta mwilini.

Dk. Kisenge aliyataja madhara yanayotokana na shinikizo la juu la damu kuwa ni mwili kupooza, shambulio la moyo, moyo kushindwa kufanya kazi, kutanuka kwa ukuta wa mishipa ya moyo, ugonjwa wa figo, kupunguza nguvu za kiume, kifo cha ghafla na kupunguza muda wa kuishi.





# DK. Shoo aonya matumizi mabaya ya fedha katika sharika

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKOFU wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, ameonya fedha za kanisa katika sharika zisitumike ndivyo sivyo.

Pia, amewahadharisha wachungaji wasikubali kuruhusu matumizi ya fedha mbichi ambazo hazijapita kwenye vitabu.

Alitoa angalizo hilo wakati wa kikao cha kwanza cha wachungaji zaidi ya 300 kutoka majimbo matano ya dayosisi hiyo, ambayo ni Kilimanjaro Mashariki, Kilimanjaro Kati, Hai, Siha na Karatu.

Kikao hicho pamoja na mambo mengine, kilikuwa kinalenga kuwakumbusha kuwa waadilifu katika masuala ya fedha, kazi na mienendo ya maisha.

"Kuna taarifa za fedha za usharika kutumika ovyo, labda unakuta mchungaji anatumia nafasi yake kushawishi watu wasiokuwa waadilifu na wasiojua wajibu wao katika Baraza la Usharika.

"Unakuta mchungaji anasema hebu nipe Sh. 100,000 hapo, pesa ambayo ni mbichi haijapita kwenye vitabu. Unapofanya hivyo ni kukosa uaminifu na unafundisha wale wengine. Hii haina baraka, taratibu za utunzaji fedha zifuatwe."

Aidha, Askofu Dk. Shoo, aliwasihi wachungaji hao kuendelea kutunza maadili ya utumishi.

"Ndugu zangu wachungaji, tumeitiwa huduma hii takatifu kwa neema ya Mungu. Ninawakumbusha na kuwasihi sana, tutunze maadili ya utumishi na haya yanaanzia na wewe mwenyewe unavyoonekana.

"How you behave (muonekano wako ulivyo), usionekana kama mchungaji wa kijiweni au mtu wa kijiweni, tafadhali!

...Utumishi huu una heshima yake, maneno yako unayozungumza yatofautiane na maneno ya kijiweni; lakini tutunze maadili ya wito wetu." alisema.

Kwenye hotuba yake, Askofu Dk. Shoo aliwataka wachungaji kuwa waadilifu katika masuala ya fedha na kuweka kumbukumbu za fedha kwa uadilifu na kufuata taratibu.

Katika hatua nyingine, Askofu Dk. Shoo alisema katika majira haya ya kipindi cha kwaresma kila mmoja ajitafakari kuhusu jambo hili linalohusu maadili ya wito wao.




Waombolezaji wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mchungaji wa kanisa la New Elim Covent (NEC), Andrea Enock Chalinze wakati lilipowasili nyumbani kwake, mtaa wa Mdote, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi na baadaye kuzikwa katika makaburi ya Potwe. Mchungaji Chalinze, alifariki dunia katika kituo cha Afya cha Kididima alipokuwa akipatiwa matibabu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TEMESA yazidai taasisi za serikali bil.1.8/- utengenezaji V8

**Na Osca Assenga,** TANGA

WAKALA wa Ufundi na Umeme nchini (TEMESA) mkoani Tanga umesema unazidai taasisi za serikali madeni sugu ya zaidi ya Sh. bilioni 1.8.

Umesema fedha hizo walikwenda kutengeneza magari yao katika karakana ya wakala huo ambapo mengine ni ya muda mrefu.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa TEMESA Mkoa wa Tanga Jairos Nkoroka wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema wanaziomba taasisi hizo kulipa madeni yao ili kuuwezesha wakala huo kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi.

Meneja huyo pia aliziomba taasisi hizo ziweze kulipa madeni yao kutokana na kwamba nao pia wanadaiwa Sh. bilioni 1.4 na wazabuni ambao wamekuwa wakipeleka vifaa kwa ajili ya kutengeneza magari

"Tunawakumbusha watulipe ili tuweze kuendelea kuwapa huduma kwani kutokufanya hivyo kunaweza kusababisha kutokupata huduma kwa wakati," alisema. Aidha alisema kwamba madeni mengi ni ya nyuma ambayo wameyarithi na mengine wameyapeleka makao makuu yao kwa utaratibu mwingine na ya mwaka huu wanaendelea kuwadai kuhakikisha wanalipa

"Tumeanzia kitengo cha mahusiano kupitia mabalozi kwa kujenga mahusiano na hivyo kusaidia wanaodaiwa kuanza kulipa madeni yao na tunaamini tutaendelea kupata mafanikio" alisema.

Aidha alisema ili kuweza kukabiliana na wadai hao sugu TEMESA umeingia mkataba na wazabuni wakubwa (40) wa vipuri vya magari mkoani Tanga ili kuondoa ucheleweshaji ambao ulikuwepo awali badala ya kuanza taratibu za manunuzi ambazo siku za nyuma zilikuwa zinawachelewesha.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kuhakikisha wanaondokana na ucheleweshwaji huo na kwa sasa wanachukua muda mfupi baada ya siku mbili.

"Hivi sasa tumeingia mikataba na wazabuni wakubwa na matengenezo ya magari ya Serikali yanatakiwa kutengenezwa na TEMESA na tukishindwa kutengeneza kutokana na kitaaluma au vifaa kuna utaratibu ambao unafahamika na tunatoa vibali kwenda kwenye karakana nyingine na yanatengezwa chini ya usimamizi wao" alisema.

Jairos alisema: "Katika suala la vifaa vya matengenezo ya magari tunatumia muda mfupi kulikagua gari na kubaini changamoto zake kutokana na uwepo wa vifaa vya kisasa".

# Silaa atatua migogoro ya ardhi 300 ndani ya siku saba

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa ametatua kero zaidi ya 300 katika wiki ya kliniki ya ardhi mkoani Arusha.

Chanzo cha kero hizo kikitajwa kuwa ni baadhi ya viongozi wasiowaaminifu kuuza eneo moja kwa watu zaidi ya 10.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa alisema kuwa baadhi ya viongozi wasiowaaminifu wamekuwa wakiuza kiwanja kimoja kwa watu zaidi ya 10.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikisababisha migogoro ya ardhi ya kudumu katika Mkoa wa Arusha.

Aidha Mtahengerwa aliwataka wananchi kuhakikisha wanapata ufafanuzi wa kutosha katika ofisi za viongozi wa mitaa ,vijiji na kata kabla ya kufanya maamuzi ya kununua maeneo Ili kuepuka migogoro ya baadaye na ambayo haina ulazima.

Alizitaka kampuni zote zinazojihusisha na biashara ya kupima na kuuza viwanja kuacha mara moja kuuza bila hati ili kuepuka migongano na kuendana na ramani ya Jiji.

"Nawasihi wananchi msiziamini kampuni hata kidogo kwa sababu hao pia ni chanzo kikubwa cha matatizo na kesi nyingi zimekuwa zikiripotiwa baada ya wananchi kuuziwa viwanja wanaambiwa kupata hati wanatakiwa wapambane wenyewe jambo ambalo ni kinyume cha sheria" alisema Mtahengerwa.

Mtahengerwa alizilaumu kampuni zinazohusika na kuuza viwanja kwamba yamekuwa yakifanya shughuli bila kuzingatia utaratibu wa mipango miji inayoonesha wapi kufanyike makazi ya watu na wapi iwe sehemu ya biashara.

Alisema kuwa migogoro mingine imekuwa ikitokana na wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa na serikali na kujimilikisha kinyume cha sheria, ambapo baada ya muda wananchi huigeukia serikali na kudai wamedhulumiwa.

Mtahengerwa pia, aliwatahadharisha watu wanaojifanya kuwa na pesa na wako juu ya sheria ambao wamekuwa wakivamia maeneo ya watu na kujenga maghorofa, akisema ikibainika siyo haki yao maghorofa yatashushwa chini ili mwenye haki amiliki eneo lake.

Alisema: "Hakuna mtu mwenye nguvu zaidi ya serikali, hata kama umejenga kwa mabilioni ya pesa kama siyo halali yako ujue umekwama na hutaendeleza ujenzi hata kama umefikia hatua za mwisho"





## Kamati yatoa maagizo H'shauri Tarime kudhibiti ufisadi

**Na Timothy Itembe,** TARIME

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeielekeza Halmashauri ya Tarime Mjini kuzingatia taratibu na hatua zote za manunuzi katika utekelezaji wa miradi, ili kudhibiti mianya ya ubadhirifu.

Pia imeiagiza kufanya ufuatiliaji kuanzia ngazi ya manunuzi pamoja na kujibu hoja za kiukaguzi zilizojitokeza na kuziwasilisha kwa wakati katika mamlaka husika.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stansalaus Mabula walipotembelea Mradi wa Ujenzi wa Soko la Kimkakati la Kisasa pamoja na ujenzi wa jengo la makao makuu ya halmashauri hiyo.

"Kuhusu mradi wa soko, tunaelekeza ukamilike kwa wakati na kukabidhiwa ifikapo Mei 17 mwaka huu kwani muda umeongezwa kwa zaidi ya mara nne nje ya mkataba. Pia tunaielekeza halmashauri kupanga vizuri bei za vizimba kwa kufanya utafiti vizuri," alisema Mabula.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Daimu Mpakate ambaye ni Mbunge wa Tunduma Kusini aliwashauri makandarasi wa mradi wa soko kuongeza nondo nene kwenye vibanda vya juu na kuweka 'ceiling board' kwa ajili ya tahadhari ya usalama.

# Mv. Mwanza yaanza majaribio ya kwanza Ziwa Victoria

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MELI ya Mv. Mwanza 'Hapa kazi tu' imefanya safari ya kwanza ya majaribio ya kiufundi katika Ziwa Victoria.

Majaribio hayo yatafanyika kwa siku tatu ili kubaini utendaji kazi wa mitambo iliyosimikwa ndani ya meli hiyo, jaribio hilo lilihusisha wataalamu 60 kutoka ndani na nje ya nchi.

Akizungumza baada ya meli hiyo kung'oa nanga katika Bandari ya Mwanza Kusini, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Eric Hamissi alisema safari hizo ni za majaribio ya kitaalamu kuelekea kukabidhiwa rasmi. "Tunatarajia kufanya majaribio haya kwa muda wa siku tatu kulingana na atakavyoshauri mkandarasi mshauri baada ya kubaini mitambo hiyo inavyofanya kazi katika ubora uliokusudiwa kabla ya kumalizia sehemu iliyobaki ili Mei 31 tukabidhiwe rasmi kama ambavyo tumekubaliana kwenye mkataba," alisema.

Hamissi alisema kukamilika kwa majaribio hayo kutapandisha asilimia za utekelezaji wa mradi huo hadi asilimia 96, huku akisisitiza kuwa zoezi hilo pekee linabeba asilimia tatu, huku asilimia nne zilizobaki zinamalizika Aprili na Mei.

Meneja Mradi, Vitus Mapunda alisema majaribio hayo yanahusisha uangalizi wa mitambo iliyofungwa ndani ya meli ili kuona ufanisi wake na ufanyaji kazi, ili kujihakikishia usalama wa meli.

Mapunda alisema meli hiyo imejengwa kumudu daraja la tatu la mawimbi katika bahari, limejengwa kumudu viwango vya bahari kuu na hata majaribio yake yanafanywa kwa kuzingatia ISO 19.

Ujenzi wa meli hiyo ulianza Januari 11, 2019 ukitarajia kukamilika Januari 10, 2021 lakini ulisogezwa mbele, kwamba hivi sasa unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa rasmi Mei 31 mwaka huu.



Mbunge wa Serengeti, mkoani Mara, Dk. Amsabi Mrimi, akizungumza na wachimbaji wadogo wa madini wa kitongoji cha Makongorosi, katika kijiji cha Majimoto, jimboni humo juzi, wanaolalamikia machimbo na mashamba yao kuchukuliwa na mwekezaji bila wao kulipwa fidia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TMDA yanasa dawa 'feki' za kuongeza nguvu za kiume

**Na Benny Kingson,** TABORA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA) Kanda ya Magharibi imekamata shehena ya dawa zenye thamani ya Sh. milioni 3.97 zinazodaiwa kuongeza nguvu za kiume.

Pia imekamata vifaa tiba vinavyodaiwa kuibiwa na watumishi wa serikali na kuviuza katika hospitali binafsi kinyume cha sheria.

Akizungumza na Nipashe kuhusu kukamatwa kwa vitu hivyo, Meneja wa TMDA Kanda, Dk.Christopher Migoha alisema dawa hizo zimo pia zinazotumiwa zaidi katika jamii, zikitajwa kuwa hatari kwa afya ya binadamu.

Dk.Migoha alisema katika operesheni waliyoifanya walikamata sigara dawa 8,642 zenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 2.1 ambako kati ya hizo sigara 2,140 zinatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) pamoja na aina ya clabu 1,038 zinazotoka India.

Alisema dawa hizo zina madhara makubwa kwa afya ya binadamu, zinasababisha ongezeko la msukumo wa damu mwilini hali inayoathiri mfumo wa upumuaji na ubongo, wakati mwingini kusababisha matatizo ya kisaikolojia.Alisema dawa nyingine zilizobainika zinatokea katika nchi za India, Burundi na Congo ambapo idadi kubwa ya dawa hizo zimemalizika muda wake wa matumizi lakini jamii imekuwa ikizinunua na kuzitumia.

Kadhalika alisema kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 walikagua mifumo 30 ya mionzi 'x-ray', m-ray na' utra sound' ambapo walibaini mifumo mitano haifanyikazi na 25 pekee ndiyo inayofanya kazi.

# Wanawake viongozi wazembe waonywa kukwamisha usawa

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wasiowajibika katika nafasi mbalimbali walizonazo wameonywa kukwamisha lengo la kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania, Lilian Liundi, alitoa onyo hilo wakati wa mafunzo kwa wanawake vijana yenye lengo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na maamuzi.

Lilian alisema ni lazima kwa wanawake kuonyesha utofauti wa uongozi kati yao na wanaume ili kuongeza idadi ya viongozi wanawake nchini. "Usitarajie kuwa wa kawaida halafu uzalishe kitu cha tofauti, hutaweza yaani kama wewe ni wa kawaida utazalisha kitu cha kawaida, lakini kama una utofauti utazalisha kitu cha tofauti" alisema.

Aliongeza: "Kitu cha kwanza cha kufikiria ni jinsi gani unajitofautisha na wengine usiende kwenye shirika fulani ukafanya 'business as usual' (kufanya jambo kwa mazoea) wewe fikiria unafanyeje iwe 'business un usual' ili uonekane tofauti".

Mafunzo hayo ya siku tatu yalishirikisha washiriki 97 wengi wao wakiwa ni viongozi wanawake katika serikali za wanafunzi katika vyuo vikuu 11 ikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu Mzumbe.

Pamoja na mambo mengine, Lilian alisema kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mabunge la Dunia (IPU) zinaonesha kuwa kuna wanawake 21 wakuu wa nchi na wakuu wa Serikali, huku kwa upande wa Afrika pakiwapo na wanawake watano waliowahi na waliopo katika nafasi za urais.

"Tumeshawahi kuwa na marais watano tu wanawake aliyekuwa Rais wa Malawi, Joyce Banda (Aprili 2012 -Mei 2014), aliyekuwa Rais wa Liberia, Ellen Johnson Sirleaf (Januari 2006- Januari 2018) aliyekuwa Rais wa Mauritius, Ameenah Gurib Fakim (Juni 2015 -Machi 2018)"

Wengine ambao bado wapo madarakani mpaka sasa ni Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde na Rais Samia Suluhu, huku idadi ya wanawake waliowahi kushika nafasi ya Spika wa Bunge ikiwa ni asilimia 20.9.

Hivyo aliwataka wanawake wenye nia ya kuongoza kujitokeza ili wapewe msaada wa kile kinachohitajika badala ya kujificha na kukaa kimya na vipaji vyao vya uongozi.

Akitoa takwimu za idadi ya wabunge wanawake nchini alisema katika wabunge wa kuchaguliwa wanawake ni 26 tu kati ya wabunge wa kuchaguliwa 264, huku wa viti maalum wakiwa ni 113 na kwamba jumla ya wabunge wanawake ni 141.

# ama


ALHAMISI MACHI 28, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Udhibiti wa EWURA bei za nishati, maji ulivyoleta nafuu kwa watumiaji**





Ukurasa 14

**DIT inapobeba dhamana kuacha mkaa ikishikwa mkono na serikali, UNDP**

MAZINGIRA

ALICHOELEKEZWA KUMALIZA MIGOGORO YA ARDHI...

# Waziri Silaa anavyomaliza papo kwa hapo, Rais amkubali anavyotekeleza

- Asifiwa hatulii, kliniki ardhi, tiba hukohuko
- Kawapa maofisa siku 100, kutimu akawaita

**Joyce Lameck na Tuntule Swebe**



Waziri Jerry Silaa, katika nyendo zake kutatua migogoro katika maeneo yenye matatizo. **PICHA: MTANDAO**

ARDHI katika jamii ni rasilimali muhimu, ambayo katika sura ya pili imekuwa ikibeba migogoro mingi ya kijamiii isiyoisha nchini. Hapo mtu anaweza kuhoji sababu zake.

Moja lililo wazi ni kwamba kutopatikana elimu sahihi ya usimamizi wake katika jamii, ikiwamo utambuzi wa mipaka sahihi.

Ni sababu mojawapo inayomfanya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi Jerry Slaa, anasimamia kuhakikisha kila haki na uhalali wake unachukua nafasi; kunavyotengwa maeneo sahihi ya ujenzi kama vile hospitali, shule, soko na viwanja vya michezo hukohuko penye mgogoro.

Nadharia iliyoko ni kama hadhira inaweza kujikita kwenye mifumo mbalimbali ya utafutaji pesa bila kusahau elimu inayotolewa, nayo inapaswa kuangukia katika darasa la mipango miji.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kimsingi, ina majukumu: Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na kusimamia upangaji wa miji na vijiji, kupima ardhi na kutayarisha ramani.

Pia, inatoa hati kumiliki na hatimiliki za kimila za ardhi; kusajili hati za umiliki ardhi na nyaraka za kisheria; kuthamini mali; kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwa na nyumba bora.

Eneo lingine linagusa kutatua migogoro ya ardhi na nyumba, kusimamia upatikanaji na utunzaji kumbukumbu za ardhi, kusimamia ukusanyaji maduhuli ya serikali yatokanayo na huduma za sekta.

Wizara pia inasimamia taasisi chini yake zikiwamo; Shirika la Nyumba la Taifa, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mengine ni Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi; Wakala wa Uendelezaji Mji Mpya wa Kigamboni; na kusimamia uendeshaji vyuo vya ardhi vya Tabora na Morogoro.

Hadi sasa katika utekelezaji huo, kuna malalamiko mengi ya watu katika maeneo wanayoyamilikii yamechukuliwa au hitilafu kisheria. Moja ya sababu ni kuwa na ardhi ziko sehemu zisizo sahihi, zimeshapangiwa na serikali kwa matumizi mengine kama barabara.

Katika jitihada zake Waziri Silaa akiwa na wastani wa miezi sita, anatatua migogoro ya ardhi kitaifa akitumia staili kuwa mbele vitani na kikosi kamili chenye majibu ya tatizo, akitolea majibu hukohuko penye mgogoro sasa mafanikio yanaanza kuonekana kwa wananchi, haki zao kupatikana.

**ALIVYOANZA KAZI**

Ni mfumo wake tangu kuteuliwa amekuwa kiongozi asiyetulia ofisini, anatembelea mikoa mbalimbali akisikiliza kero za migogoro ya ardhi ambayo ni kilio kikubwa kitaifa, hasa kwenye suala la mirathi, hata kutokeza mikasa isiyo ya kibinadamu.

Agizo lake kwa maofisa ardhi ikawa kuacha kuwa washauri kisheria kwa wananchi, bali watendaji kitaalamu.

Kwa historia yake, Waziri Silaa alianza kazi Septemba mwaka jana katika wadhifa wa sasa akiahidi wizara yake "Itahakikisha kero zote za migogoro ya ardhi zinakwisha, ikiwamo jijini Dodoma."

Akaitaja kuwa sehemu ya utekelezaji rasmi wa maagizo kwake ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni tamko lake la Novemba iliyopita, kwa wananchi waliofika katika alichokibuni 'kliniki ya ardhi' anayoiendeleza hadi sasa

Waziri huyo akawaambia wananchi waliofika kupata huduma katika kliniki hiyo kuwa, atakuwa akifanya nao mazungumzo kila baada ya kumaliza ratiba za bunge, ili kujionea mwenyewe kero zinazowakabili za ardhi.

INAENDELEA UK.13

AFYA

# Udhibiti wa EWURA bei za nishati, maji ulivyoleta nafuu kwa watumiaji

**Na Mwandishi Wetu**

MAFANIKIO ya kiuchumi ni mchakato wa mabadiliko kutoka chini kwenda juu ambao unatokana na ushiriki wa moja kwa moja wa wananchi kwa kushirikiana na serikali na sekta binafsi ikiwamo kutumia fursa za kiuchumi zilizopo kwa wakati husika.

Maendeleo ya kiuchumi katika nchi huletwa na mambo mengi lakini kubwa zaidi ni watu kufanya kazi kwa bidii pamoja na taasisi za kimaendeleo, zikiwemo za serikali na za binafsi, kuwawezesha wananchi kutambua na kuzitumia vizuri fursa zilizoko katika maeneo yao.

Moja ya taasisi za serikali ambazo zinachangia katika kuleta maendeleo ni mamlaka za usimamizi kama Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ambazo zimepewa jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za kiuchumi na kijamii. Lengo ni kuhakikisha huduma hizo zinawafikia moja kwa moja wananchi.

Mamlaka hizi zinahusika moja kwa moja na kusimamia na kuratibu shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwamo kudhibiti wa kiufundi na kiuchumi. Udhibiti wa kifundi ni pamoja na unadhifu wa miundombinu na ubora wa huduma kupitia utoaji wa leseni na udhibiti wa kiuchumi ni pamoja na kulinda mitaji ya watoa huduma na maslahi ya watumiaji huduma ikiwamo upangaji wa bei za huduma.

EWURA ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya mwaka 2001 (Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania) pamoja na majukumu mengine, kupewa majukumu chini ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 (Sura ya 392) kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa petroli (mafuta na gesi asilia) Tanzania Bara.

Kazi kubwa ya mamlaka hiyo ni kutoa leseni za uendeshaji wa shughuli za nishati na maji nchini, mapitio ya gharama za uendeshaji wa huduma, kufuatilia utekelezaji wa viwango vya ubora, usalama, afya na mazingira. Pia ina wajibu wa kukuza na kuendeleza ushindani wenye tija kiuchumi, kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma pamoja na kuendeleza upatikanaji wa huduma zilizowekwa kwa watumiaji wote wa kipato cha chini, watumiaji wa vijijini na wasiostahili katika sekta zilizosimamiwa.

EWURA pia inadhibiti shughuli za gesi asilia zinazojumuisha usafirishaji, uhifadhi na usambazaji.



Rais Samia Suluhu Hassani, akikata utepe kuzindua Ripoti ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini, ambayo huandaliwa na EWURA kuchambua utendaji wa mamlaka za maji za mikoa, wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa katika kuchochea utoaji wa huduma ya maji nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

> **Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, anasema EWURA haitavumilia wanaofanya biashara ya mafuta katika vituo bubu na maeneo mengine yasiyoruhusiwa.**

Miundombinu ya gesi asilia kama mitambo ya kusindika gesi, mabomba ya upitishaji na usambazaji pia vinadhibitiwa na mamlaka ili kuhakikisha kunakuwa na ubora wa huduma huku utunzaji wa mazingira ukipewa kipaumbele cha hali ya juu.

Mamlaka inajitahidi kuboresha ustawi wa jamii ya Tanzania kwa kukuza ushindani mzuri na ufanisi wa uchumi, kulinda maslahi ya watumiaji, kulinda uwezo wa kifedha wa watoa huduma ili kusambaza bidhaa kwa ufanisi.

Pia ina jukumu la kukuza upatikanaji wa huduma zilizodhibitiwa kwa watumiaji wote pamoja na wenye vipato vya chini, watumiaji wa vijijini na wanyonge, kuzingatia umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira, kuongeza uelewa kwa umma juu ya huduma zinazodhibitiwa.

**ILIVYOKUWA KABLA**

Kabla ya kuanzishwa mwaka 2006, taasisi kama Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira na kampuni zinazofanya biashara ya mafuta, zilikuwa zikipanga bei ama kwa utashi wa wafanyabiashara au menejimenti ya taasisi husika.

Kutokana na kukosekana kwa udhibiti, bei za huduma kwa rejareja kama mafuta, zilipanda holela, hivyo kuwaumiza watumiaji huku wafanyabiashara wakitumia mwanya huo kuwakandamiza wateja.

Kwa mfano, baada ya kuona kuwa bei za mafuta zinapanda holela pengine hata mara tatu kwa siku, Januari 2009, EWURA iliingilia kati kwa kuanza kutoa bei kikomo. Dar es Salaam bei ilishuka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 1,233 kwa lita ikiwa ni punguzo la asilimia 62. Kwa mikoa ya mbali kama Kigoma, bei ilishuka kutoka takribani Sh. 2,400 hadi Sh. 1,642 kwa lita ikiwa punguzo la asilimia 52.

Kuanzishwa kwa EWURA kuliwezesha taasisi zote kuheshimu sheria, kanuni na taratibu na kufuata hatua mbalimbali ikiwamo kushirikisha wadau, hususan watumiaji wa bidhaa husika kama vile umeme na maji.

Kwa sasa, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, TANESCO au kampuni binafsi ya kuzalisha umeme, kama inataka kurekebisha bei ni lazima ipitie hatua mbalimbali ikiwamo kuwasilisha maombi EWURA, kufanya mikutano na wadau ili kuwashirikisha kuhusu nia ya kurekebisha gharama ya huduma na wadau kutoa maoni yao kama ni kupinga au kukubali.

Taasisi husika pia ni lazima ieleze sababu za kusudio la kurekebisha bei. Katika kufuata hatua hizo, TANESCO imeshuhudiwa ikianzisha mchakato wa kutaka kupandisha bei za umeme kwa wateja wake. Shirika hilo lilifuata taratibu zote ikiwamo kufanya mikutano na wadau kupitia Baraza la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA-CCC).

Mikutano hiyo iliyofanyika maeneo mbalimbali nchini, ilitoa fursa kwa watumiaji wa huduma hiyo kupinga nia ya kupandisha bei ya umeme. Kwa mantiki hiyo, taasisi inapotaka kupandisha bei ni lazima ihusishe wadau ili nao watoe maoni kabla ya hatua zaidi kufuata ili kutimiza lengo lililokusudiwa.

Hata bei za mafuta, kutokana na udhibiti makini wa EWURA, zimekuwa zikitangazwa kila mwezi huku zikionyesha wakati mwingine kushuka kulingana na sababu mbalimbali kama vile bei katika soko la dunia kushuka. Kuwepo kwa EWURA pamoja na mabadiliko ya bei za mafuta kumepunguza maumivu kwa watumiaji wa mafuta kwa asilimia 30 ikilinganishwa kama EWURA isingekuwepo.

Kuwapo kwa udhibiti huo, kumesaidia kuwapunguzia mzigo wananchi wanaotumia mafuta kwa shughuli mbalimbali na kuwabana wafanyabiashara waliokuwa wakifanya njama za kupanga bei kwa utashi wao, hivyo kuwaumiza watumiaji wa mafuta.

Pia kuwapo kwa EWURA kumewafanya wafanyabiashara waliokuwa wakigoma kuuza mafuta wakisubiri mafuta yaadimike ndipo wapandishe bei, kutofanya hivyo na wale waliokiofanya hivyo walikumbwa na fagio zito la chuma kwa kupewa adhabu kali.

EWURA ina nafasi kubwa katika kuleta maendeleo hapa nchini kwa mfano, kwa utoaji wa bei kikomo kwenye mafuta, Watanzania wanapata nafuu kwa bidhaa ukilinganisha na kabla ya uwepo wa EWURA. Kwa hiyo fedha iliyobaki inatumika kwenye matumizi mengine ya kimaendeleo.

**FAIDA YA VINASABA**

Uanzishaji wa kuweka vinasaba kwenye mafuta umeifanya serikali kupata faida kubwa. Utafiti wa Chuo Kikuu ch Dar es Salaam ulionyesha kuwa kati ya mwaka 2010 na 2013 ulibaini ongezeko la mapato ya serikali (kodi) kwa Sh. bilioni 468.50 ikiwa ni Sh. bilioni 146.5 (2010/11), Sh. bilioni 129.8 (2011/12) na Sh. bilioni 192.2 mwaka 2012/13.

Katika mapambano dhidi ya soko holela la mafuta, udhibiti wa ubora wa mafuta ya petroli na gesi asilia, EWURA imeendelea kudhibiti wa uuzwaji holela wa bidhaa za mafuta aina ya petroli, kwa wanaofanya biashara hiyo kinyume cha sheria.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, anasema EWURA haitavumilia wanaofanya biashara ya mafuta katika vituo bubu na maeneo mengine yasiyoruhusiwa.

**INAENDELEA UK.13**

MAZINGIRA

# Waziri Silaa anavyomaliza papo kwa hapo, Rais amkubali anavyotekeleza

**INATOKA UK.11**

Silaa akawaelekeza watendaji wa sekta ya ardhi nchini, kuhakikisha ndani ya 100 kuanzia Septemba mwaka jana aingie katika jukumu hilo, wanatatua migogoro ya ardhi kwa nafasi zao.

Aidha, akawataka waliovamia maeneo ya wazi kuanza kuondoka mara moja huku akielekeza viongozi na watendaji wa Wizara ya Ardhi wenye mamlaka ya kusimamia sheria katika maeneo mbalimbali, ya wazi.

Hilo akalitolea ufafanuzi, huku Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga, akinena kuwa 'Kliniki ya Ardhi, itakuwa mwarobaini wa changamoto nyingi zinazowakabili wananchi wengi,' akitumia mfano wa jijini Dodoma.

Hapo ndipo akatangaza kutanua wigo na ziara za mbali, akiwa na ufafanuzi: "Kliniki ya Ardhi kwa sasa iko Dodoma na ni endelevu kwa mikoa yote.

"Pia, wizara inakusudia kuweka mifumo rahisi ya kutoa huduma kwa wananchi, ikiwamo kufunga kamera katika ofisi za utoaji huduma ili kuepuka mianya ya ukiukwaji sheria."

Kila anapokuwa ziarani kuendeleza mkakati huo, Waziri Silaa, amekuwa mbunifu kulingana na mazingira. Mathalan mkoani Kilimanjaro miezi kadhaa baada ya uteuzi wake, akiunda kamati za kukusanya taarifa kutatua migogoro ya ardhi katika vijiji vya Bangalala, Mwembe na Makanya vilivyopo wilayani Same.

Hiyo ni baada ya kufanya mkutano wa hadhara na wanakijiji, akiongozana na Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni kutatua migogoro ya umiliki wa ardhi.

Ni kamati iliyoundwa na wawakilishi wa wananchi vijijini, Kamishna wa Ardhi kutoka Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Same na wataalamu ardhi, ili apate uamuzi sahihi lwa suala hilo.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, akiwa katika mkutano wa kutatua migogoro ya ardhi katika vijiji vya Bangalala, Mwembe na Makanya, wilayani Same Mkoani Kilimanjaro, Januari mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

**CHANGAMOTO MBELE YAKE**

Katika ziara zake ambazo zinamng'arisha sasa kiutendaji Silaa, anakabiliwa na uhaba wa rasilimali watu na fedha, anakosa taarifa sahihi za miliki ya ardhi na uchelewashaji wa malipo ya fidia.

Mengine inatajwa ni kulimbikizwa kodi ya pango la ardhi, migogoro, uvamizi wa ardhi, kasi ndogo ya upangaji na upimaji ardhi, ikilinganishwa na uhitaji uliopo kwa kwa jili ya matumizi mbalimali.

Anataja hatia zake ni serikali inahakikisha viwanja vyote vilivyopimwa vinamilikishwa kwa wahusika, kukiongezeka kasi ya uandaaji mipango ya matumizi ya ardhi, kuwekwa utaratibu bora mzuri wa mgawanyo wa fedha zinazohitajika kutumiwa.

**MTAZAMO WA WADAU**

Baadhi ya wananchi wanatoa maoni yao wakimpongeza waziri huyo wakitambua namna anavyotatua migogoro ya wananchi kwenye maeneo mengi, hata wanatoa rai aigwe na viongozi wengine.

Rashid Mkumba, anasema: "Kwa kweli anawasaidia sana watu ambao walikuwa kwenye migororo ya ardhi, amekuwa akifanya kazi bila kuangaalia mazingira mjini, vijijini kote. Anafanya kazi hivyo jitihada zake zimekuja na mafanikio kwa wengi."

Mwingine Agustino Njana, anaunganisha: "Huyu ni kiongozi wa kuigwa kwa sababu anafanya kazi usiku na mchana, wakati wengine wanakaa kwenye ofisi zao bila kujali wananchi wana changamato kiasi gani, lakini Silaa anazungukua na kufuata migogoro ilipo na kuhakisha anawapa majawabu sahihi tena kwa haki."

**SIKU 100 KAZINI**

Kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ikawa na ufafanuzi ufuatao siku alipotimiza siku 100 kazini, mnamo Desemba 21, mwaka jana, Waziri Silaa akafa ya kikoa na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi mikoa yote Tanzania Bara, kutathmini siku 100 za uongozi wake, kujitathmini katika kutekeleza maagizo ya Rais Dt. Samia Suluhu Hassan kuhusu matumizi bora ya ardhi.

"Hiki ni kikao kazi cha kutathmini siku 100 na kutengeneza mpango wa kutekeleza maagizo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutatua matatizo ya migogoro ya ardhi na kuwahudumia wananchi wetu," akatamka Waziri Silaa.

Hapo akawasisitiza Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa, kwamba wana kazi ya kusimamia watumishi chini yao kujipanga vizuri na wana uwezo kubadilisha jinsi sekta ya ardhi inavyoendeshwa nchini kote.

Waziri Silaa akanena kuwa, Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wanachapa kazi katika mikoa yote na utendaji wao ndio unatoa taswira inaopaswa kusonga, kutekeleza maelekezo ya viongozi wa kitaifa, kuleta tija kwa Watanzania.

Aidha, Waziri Silaa akawaambia kuwa wizara yake itaendelea kushirikiana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kupokea na kuheshimu ushauri wanaoutoa kuhusu shughuli za sekta hiyo nchini.

**ANAVYOPOKEWA IKULU**

Rais Samia Suluhu Hassan, mnamo wiki mbili zilizopita akizungumza Ikulu, Dar es Salaam, alieleza kufurahishwa na juhudi zinazofanywa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kupita kwa wananchi kusikiliza kero zao na kuzitatua paopo kwa hapo.

Akatamka: "Nafurahishwa na juhudi zinazochukuliwa sasa hivi na Wizara ya Ardhi kupita na kusikiliza kero na kuzitatua palepale lakini Wizara ya Ardhi ni moja... Wakuu wa Mikoa wasaidieni angalau wakija wanakuta mmeshafanya, wao wanatoa suluhisho."

## Udhibiti wa EWURA bei za nishati, maji ulivyoleta nafuu kwa watumiaji

**INATOKA UK.12**

"Kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na adhabu yake ni kulipa faini kiasi kisichozidi Sh. milioni tano au kifungo cha miaka mitatu jela," anasema.

EWURA pia imepania kuendelea kudhibiti mkondo wa chini wa sekta ya petroli kwa kuhakikisha inaondoa mianya yote ya wizi, watumiaji wa bidhaa hizo wapate huduma iliyobora, kulinda afya pamoja na mazingira kwa maendeleo.

Katika mwendelezo wa jitihada hizi za kupambana na soko holela la mafuta, EWURA imeviadhibu vingi vya mafuta kwa kufanya biashara bila leseni ya EWURA, kujengwa bila vibali na kutokidhi viwango vya ubora vya utoaji huduma ya mafuta.

"Usione vituo vya mafuta siku hizi vinapendeza sana hata ukitoka eneo la kituo hujulikani tofauti na huko nyuma ambapo ungekuwa unanuka mafuta. Ubora huu umetokana na usimamizi mzuri wa EWURA", anasema Dk. Andilile.

EWURA hufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo vya mafuta kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vya ubora, kulinda afya na kuzingatia usalama wa afya na mazingira ya Watanzania kwa kuchukua hatua vituo vinavyokwenda kinyume cha taratibu.

Uuzaji wa mafuta yasiyo na vinasaba ni mwanya wa ukwepaji kodi na ni uhujumu uchumi wa nchi, hivyo EWURA imekuwa ikisimamia suala hili kwa umakini mkubwa. Udhibiti wa ubora wa mafuta ya petroli.

Moja ya majukumu ya msingi ya EWURA ni kuhakikisha wafanyabiashara ya mafuta wanafuata sheria, kanuni na kukidhi viwango vya ubora katika utoaji huduma za mafuta nchini.

Sheria ya EWURA na Sheria ya Petroli zinaipa EWURA mamlaka ya kudhibiti masuala ya kiufundi, kiuchumi na kiusalama katika sekta ya petroli.

EWURA husimamia wauzaji wa jumla na rejereja wa mafuta ili kuhakikisha wanatoa huduma yenye ubora na viwango vinavyostahili na kwa gharama ambayo watumia huduma hiyo wanaimudu.

Mamlaka pia ina jukumu la kuhakikisha kuwa mafuta yanayotumika nchini yanakidhi viwango vya ubora kama vilivyoanishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kabla mafuta haliyopokewa kutoka nje ya nchi hayajaingia katika matumizi. Wafanyabishara ya mafuta nao wana wajibu wa kuhakikisha kuwa bidhaa zao wakati wote zinazingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

Hilo hufanyika kwa kufanya ukaguzi kujiridhisha kuwa taratibu za kisheria na kanuni za uendeshaji biashara zinafuatwa kikamilifu. Mamlaka huchukua sampuli za mafuta ili kujiridhisha endapo bidhaa za mafuta zilizo sokoni zinakidhi viwango vya ubora na ni salama kwa matumizi.

MAZINGIRA

# DIT inapobeba dhamana kuacha mkaa ikishikwa mkono na serikali, UNDP

• Uhalisia; pamoja na kuni zimeshika kote

**Na Maulid Mmbaga**

WATANZANIA takribani 33,000 mijini na vijijini, wanaelezwa kuwa wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na matumizi ya nishati chafu inayohusisha kuni, mkaa na vinyesi vya wanyama kama ng'ombe kupikia.

Idadi hiyo inayopotea ni kutokana na kuumwa maradhi yanayoshambulia mfumo wa hewa unaohusisha koo, mapafu, pia na midomo wakati mwingine wakiumwa saratani na kichomi.

Vifo na athari hizo ni matokeo ya kutumia nishati chafu kwa miaka mingi, vinaelezwa na mtaalamu wa matumizi bora ya nishati kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Sayuni Mbwilo, katika mazungumzo na Nipashe.

Anasema, chanzo cha magonjwa na vifo ni vumbo na moshi unaotokana na kutumia kuni, mkaa, mabaki ya mimea, vinyesi vya ng'ombe na mbuzi.

Aidha, kwa mujibu wa Wizara ya Nishati, takriban asilimia 85 ya Watanzania wanatumia nishati ya kuni, mkaa, mabaki ya mazao na vinyesi vya wanyama, huku asilimia 72 ya nishati yote iliyoko nchini ikitumika majumbani na si viwandani au kwenye usafirishaji.

Katika kutekeleza mradi wa kubadilisha matumizi ya nishati duni, serikali na wadau wanamlenga zaidi 'mama' .

Wizara ya Nishati, UNDP, Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) wamechukua hatua za kimkakati kutafiti na kutoa suluhisho la kuepukana na nishati chafu jikoni.

Hapo ni kuhamasisha jamii hasa wanawake kuachana na kutumia kuni na mkaa jikoni na kuhamia kwenye gesi, umeme na mkaa mbadala ni moja ya mikakati hiyo, ambayo itafanikisha kutunza mazingira na kulinda afya za wananchi.

Sayuni anafafanua kuwa, Watanzania hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi, kama gesi, umeme, sola, mkaa mbadala na au vimiminika kama 'etheno'.

Anasisitiza elimu hiyo ni muhimu kwenye nishati, kwakuwa ikikosekana watu hawataelewa jinsi jiko sanifu linavyosaidia kuepuka matumizi ya kuni, mkaa au mabaki ya mimea kupikia ambayo pamoja na kudhuru mapafu na koo, pia huchangia uharibifu wa mazingira na tatizo la mabadiliko ya tabianchi.

Anazungumzia hatua zinazochukuliwa na UNDP akitaja kugharamia masomo ya wanafunzi wa kike 10 kujifunza mafunzo ya nishati safi kwa ngazi ya shahada katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na kwamba, baada ya kuhitimu watatumika kukuielimisha jamii umuhimu wa nishati salama.



Wauzaji mkaa, Mbande, Dar es Salaam wakisubiri wateja. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Jiko la mkaa.

> **Cha kwanza ni mtu aelewe na aone maana ya kuhusika kwasababu hili ni jambo linalohusisha kila mmoja wetu na pia maisha yetu.**

Pamoja na mafunzo, DIT imepokea vifaa vya kisasa vya kufundishia pamoja na kupima ufanisi, viwango na matumizi sahihi ya majiko hayo.

"Wanawake 10 watakwenda kuvitumia vifaa hivi kujua namna gani wanamsaidia Mtanzania, hasa mama ile nishati yake safi ya kupikia isipotee bali itumike kwa ufanisi, umakini na ubora," anasema Sayuni na kuongeza Ubalozi wa Ireland, umeongeza msaada wa uhisani wa masomo kwa wanafunzi wengine 10 wanawake

Mmoja wa wanafunzi wanufaika wa ufadhili huo, Sherida Magomere, anasema ujuzi watakaopata utawaelimisha Watanzania umuhimu wa nishati salama ya kutumia katika shughuli za kila siku na hasara za nishati chafu ili waepuke madhara.

Mkufunzi Mwelekezi kutoka DIT, Mawazo John, anasema, kuanza kwa mradi huo kumeleta mwamko kwa wanafunzi wa kike kujiongezea uelewa katika eneo la nishati safi, akibainisha awali katika darasa nzima wanawake walikuwa wanne pekee, lakini mwaka huu wako zaidi ya 40 wakiwemo wanaogharamiwa na UNDP.

Augustino Masse, mtaalamu wa teknolojia za nishati kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), anasema jamii inahitaji elimu ya kutambua inaathirika vipi na nishati isiyo safi.

Hapo anatoa mfano wa afya kwamba, inachukua miaka mingi kupata athari za moshi na vumbi jembamba analivuta mtu kutoka kwenye kuni, mkaa na mabaki ya mimea, kwenye shughuli zake.

"Leo anaweza asione kwamba nishati safi ni kitu muhimu, lakini tukielimisha jamii ipasavyo, unaposema nishati safi unamaanisha nini tutafikia lengo.

"Cha kwanza ni mtu aelewe na aone maana ya kuhusika kwasababu hili ni jambo linalohusisha kila mmoja wetu na pia maisha yetu," anaeleza Masse.

"Mimi ni mtaalamu lakini kama mwananchi haelewi umuhimu wa hili utaalamu wangu utakuwa haujafanya chochote, ndio maana nasisitiza cha kwanza ni elimu na uelewa kwa jamii.

'Chini ya mradi huu kuna kipengele kimewekwa mahususi kwamba watu waelimishwe, kwenye viwanda, nyumbani na kote ambako nishati inatumika," anaongeza.

Anasema pamoja na kuhimiza kuacha kuni na mkaa, TIRDO imefanya tafiti na kubaini namna bora ya kutengeneza mkaa mbadala, utaalamu wanaoendelea kuupelekea kwa Watanzania wengine maeneo mbalimbali.

### UHAKIKI MAJIKO

Mtaalamu huyo wa teknolojia kutoka TIRDO, anasema nishati safi, inaanzia kwenye jiko, akibainisha Shirika la Viwango Tanzania (TBS), majiko yanatakiwa kuwa katika daraja la kwanza yakiwa na ufanisi wa asilimia 50, la pili zaidi ya asilimia 40 na tatu zaidi ya asilimia 30, nne kuanzia asilimia 20 hadi 29.

Anasema, kutokana na viwango hivyo wanaendesha zoezi la uhakiki ubora na kuwasaidia na kuwashauri namna ya kuboresha majiko yao.

Winifrida Robert ni Mhandisi wa Nishati kutoka TIRDO, anayesema wanawake wengi wanapata madhara ya kiafya na kuingia gharama kubwa za matibabu, kwa kutokujua ufanisi wa jiko analolitumia na kusisitiza uelewa wa suala hilo kuwa ni muhimu kusaidia kutumia nishati kwa kiwango.

"TIRDO kwa kushirikiana na UNDP imetengeneza maabara yenye vifaa vya kisasa vinavyotumika kupima ufanisi na hewa ukaa ambayo inatoka kwenye jiko, wazalishaji wengi hawajui maana ya kupima ufanisi wa jiko, pia wanunuzi hawaelewi kuna faida unayoipata kwa kununua jiko lenye ufanisi.

"Chini ya mradi tumewafikia baadhi ya wajasiriamali na wameleta majiko yao kupimwa, hivyo nitoe wito kwa wazalishaji wengine kufika TIRDO kupima ufanisi na tutawapa ushauri kuongeza thamani ya bidhaa zao. Pia watu kabla ya kununua wajiridhishe kuhusu ubora,"anashauri Winifrida.



# Madaktari watoa ushauri uboreshaji Bima ya Afya kwa Wote

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI mkazi wa Shirika la Pharm Access, Dk. Heri Marwa, amesema ili mpango wa Bima ya Afya kwa Wote (UHC) uwe na ufanisi katika huduma za afya ya uzazi, serikali inapaswa kutengeneza kadi maalum kwa wajawazito, kuwawezesha kuhoji huduma wanazopata kwenye vituo vya kutolea huduma.

Alitoa ushauri huo jana jijini hapa, wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Afya Msingi kuhusu ugharamikiaji wa huduma ya uzazi kwenye UHC.

Alisema katika utekelezaji wa Sheria ya UHC ni muhimu kuwalinda watu ambao wapo kwenye hatari ambao ni pamoja na wanawake na watoto wachanga.

Dk. Heri alisema tatizo kubwa hivi sasa ni mfumo ambao unatumika kulipia huduma za afya kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano, ambao ni wa kupeleka vitenganishi na dawa kwenye vituo vya afya.

"Ukiangalia dunia nzima mfumo huu umekuwa na changamoto nyingi hasa upande ufanisi, unakuta wanawake wanafika pale wanaambiwa huduma hazipo ama hazipatikani na mwisho wanaambiwa wakalipie kwenye sehemu zinakopatikana," alisema

Aidha, alisema kwa mfumo ambao wameufanyia majaribio katika Mkoa wa Manyara kila mjamzito anakuwa na kadi kama ya bima ya afya ambayo inamwezesha kwenda popote anapotaka kupata huduma, huku kituo husika kikilipwa kutokana na walivyomuhudumia.

Kadhalika, alisema wameanza mazungumzo na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ili kufanya majaribio kwa eneo kubwa la Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Pia, alisema wanaamini kama mama akipewa kadi hiyo badala ya kumweleza kuwa atapata huduma ya bure hospitali, itasaidia huduma zote anazotakiwa kuzipata na kituo kitakuwa hakina shida ya ukosefu wa raslimali fedha.

Akielezea jinsi mfumo wa kutumia kadi kwa wajawazito ulivyoweza kuboresha huduma za afya, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Magugu wilayani Babati, mkoani Manyara, Dk. Costa Ndunguru alisema walianza kutumia mfumo huo Mei mwaka 2019, kwamba umeonyesha ufanisi.

Alisema mradi huo unaoendeshwa na Shirika la Pham Access, unatoa kadi yenye Sh.104,000 kwa wanawake wanaotoka katika familia masikini ambapo kila wanapohudhuria kliniki na kupata huduma hukatwa gharama.

"Kabla hajaja anapokea ujumbe mfupi katika simu yake ya mkononi kumweleza juu ya huduma anayokwenda kuipata katika siku husika kliniki, asipoipata anaidai, akiambiwa haipo basi anakwenda katika kituo kingine anapoweza kuipata," alisema.

Alisema hali hiyo imesaidia pia wajawazito kupata huduma stahiki ukilinganisha na awali ambapo wakati mwingine walikuwa hawapati vipimo vyote muhimu walivyokuwa wakivihitaji kwa usalama wao na watoto wao.

Dk. Ndunguru alisema utekelezaji wa mfumo huo umeongeza mahudhurio ya wajawazito chini ya wiki 12, kutoka asilimia 16 hadi 50, huku wanaohudhuria zaidi ya mara nne wakiongezeka kutoka asilimia 25 hadi 80.

"Pia kinamama wanaojifungulia katika kituo hicho wameongezeka kutoka 100 hadi 120 kwa mwezi, huku wanaohudhuria kliniki nao wakiongezeka kutoka 140 hadi 170 kwa mwezi" alisema.

Kadhalika, Dk. Ndunguru alisema mfumo huo umewawezesha kuboresha huduma katika kituo hicho kwa kuongeza vifaa, dawa na wamefungua duka la dawa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Philip Besiimire (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kulia), wakipiga makofi baada ya kuzindua ushirikiano kati ya taasisi hizo, jijini Dar es Salaam jana, utakaowezesha upatikanaji wa simujanja kwa mkopo ili kuchochea matumizi ya intaneti na ukuaji wa uchumi wa kidijiti nchini. Kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom, Linda Riwa na Ofisa Biashara Mkuu wa benki hiyo, Boma Raballa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SUWAZA yatwishwa zigo usimamizi mabwawa majitaka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) kusimamia kwa karibu mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka unaojengwa katika Manispaa ya Singida kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya kutembelea mradi huo ambao unajengwa eneo la Manga, ambapo alisema serikali imetoa fedha nyingi kutekeleza mradi huo, hivyo hategemei baada ya muda mfupi uharibike kutokana na kutojengwa vizuri.

"Meneja wa SUWASA msimamie mkandarasi ahakikishe anajenga mradi vizuri ili thamani ya fedha ionekane.

Hatutegemei mradi ukae muda mfupi uanze kuharibika, nawapongeza manispaa kwa kupata mradi kama huu,"alisema.

Awali akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa, Meneja wa SUWASA, Sebastian Warioba, alisema mradi huo umeanza kujengwa Mei mwaka jana na unatarajia kukamilika Novemba mwaka huu na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 46.

Warioba alisema kujengwa kwa mradi huu ni ukombozi mkubwa kwa Manispaa ya Singida kwani kwa kipindi kirefu majitaka yalikuwa yakielekezwa porini jambo ambalo kiafya sio zuri

Warioba alisema Singida imebahatika kuwekwa katika mpango wa mradi wa miji 10 ambayo utawezesha kujengwa kwa mtandao wa majitaka kwa kujengwa kutoka kwenye majumba.

Mkuu wa Mkoa akiwa katika mradi wa Kituo cha Afya Mtipa, aliipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwa kujenga kituo hicho kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani zaidi ya Sh. milioni 500.

Dendego alisema yeye pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe kituo hicho kitakapokamilika watapambana kuhakikisha vifaa tiba vinapatikana ili huduma za matibabu zianze kutolewa haraka.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alisema kituo hicho kilianza kujengwa Februari 2023, kinatarajia kukamili Mei na kitatoa huduma kwa wananchi wa Kata ya Mtipa na kata jirani.

# Serikali yapewa mbinu kupunguza vifo, ulemavu wa kudumu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuendelea kuwekeza na kutoa huduma za dharura katika ngazi ya afya msingi, ili kupunguza vifo na ulemavu wa kudumu unaotokana na majeruhi.

Ushauri huo ulitolewa na mtaalamu kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dk.Karima Khalid wakati wa mkutano wa kwanza wa kimataifa wa afya ya msingi uliohusu umuhimu wa huduma za dharura (EECC).

Alisema tayari Tanzania ina mpango mkakati wa miaka minne wa huduma za dharura ambao unalenga kuimarisha huduma hiyo.

Alisema katika utafiti uliofanywa kuangalia huduma hizo hapa nchini unaonesha asilimia 85 ya hospitali rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya EECC zinapatikana lakini katika kituo asilimia 57 ya rasilimali zinazohitajika zipo tayari kutumika kwa mgonjwa mahututi.

"Huduma za mahututi ya hali ya juu hazitoshi kutolewa kwenye hospitali kutokana na asilimia 31 ya rasilimali ndio zinapatikana katika kiwango cha hospitali, mafunzo na ununuzi wa vifaa ni muhimu lakini haitoshi kama suluhisho la jumla," alisema.

Alitaja faida za kuwekeza katika huduma hiyo ni kusaidia kuboresha huduma na kuokoa maisha ya wagonjwa mahututi katika ngazi ya afya msingi.

Mtaalamu mbobezi wa huduma hiyo, Dk.Erasto Slyvanus , alisema wagonjwa mahututi wanapaswa kupata tiba sahihi na rasilimali zilizopo zitunzwe na kutumika kuokoa maisha ya wagonjwa hao.

Alisema hadi sasa asilimia 83 ya hospitali za wilaya na hospital zote za rufaa za mikoa zina idara ya huduma za dharura.



# Mafuriko yasababisha kaya zaidi ya 60 kukosa makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NYUMBA tatu zimebomoka na zingine zaidi ya 60 kuzingirwa na maji na kusababisha wananchi kukosa makazi katika kata mbili mkoani hapa baada ya mito na mifereji kufurika kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Kata zilizoathirika na mafuriko hayo ni Isyesye na Sinde ambako maji yamehama kwenye njia kutokana na ujenzi holela wa makazi pamoja na uharibifu wa mazingira.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao akiwemo Elizabeth Mwaseba mkazi wa Mtaa wa Vingunguti alisema mafuriko hayo yamewatesa kwa zaidi ya wiki na kwamba wanashindwa kutoka na kuingia kwenye nyumba zao kutokana na kuzingirwa na maji.

Alisema mvua ilianza kunyesha majira ya jioni mpaka usiku na kwamba wakiwa wamelala saa 4:00 usiku walisikia kelele za maji na walipoamka wakabaini kuwa maji yalikuwa mengi na yanaingia kwenye nyumba zao.

Elizabeth alisema awali waliamini kuwa maji hayo yangeondoka lakini yakaendelea kuingia na kujaa na kwamba hata watoto wanashindwa kwenda shuleni kutokana na njia kutopitika.

Naye James Mwaipungu alisema chanzo cha mafuriko hayo ni uovu wa miundombinu ya mitaro pamoja na ujenzi holela ambao umesababisha maji kukosa njia na kuingia kwenye makazi ya watu.

Alisema baadhi ya watu wamejenga nyumba katika mapito ya maji na hivyo kusababisha maji kushindwa kufuata mkondo na kuvamia nyumba.

Hivyo, aliiomba serikali kupitia maofisa ardhi kupanga vizuri makazi ya wananchi katika eneo hilo na kuweka vizuri mifereji ya maji ili maji yasiendelee kuvamia makazi.

Emma Amfred alisema kwa sasa wanashindwa kufanya shughuli zao za maendeleo kutokana na kushindwa kupita kwenye maji pamoja na kuogopa kuwaacha watoto pekee yao.

Alisema wanahofia kuwaacha watoto wao nyumbani na wakaenda kufanya shughuli zao watoto wao wanaweza wakasombwa na maji na kudhurika.

Diwani wa Kata ya Isyesye, Ibrahim Mwampwani alisema kutokana na mafuriko hayo kuvamiwa na maji, serikali imeanza kujenga mtaro wa maji ambao utasaidia kuondoa mafuriko hayo na kunusuru makazi ya wananchi.

Alisema kata hiyo ni miongoni mwa maeneo yanayonufaika na mradi wa kuboresha miundombinu (TACTIC) na kwamba katika utekelezaji wa mradi huo kata hiyo ipo katika awamu ya pili ambayo utekelezaji wake bado haujaanza.

Alisema pamoja na kwamba utekelezaji wake bado lakini baada ya kuvamiwa na mafuriko serikali imepeleka katapila ambalo tayari limeanza kuchimba mtaro ili kuondosha maji yaliyoko kwenye makazi ya wananchi.



Maofisa wa Taasisi ya Tulia Trust, wakikagua baadhi ya nyumba za wananchi zilizobomoka kutokana na mafuriko katika mtaa wa Sinde A, Kata Sinde jijini Mbeya juzi walipokwenda kwa ajili ya kuwafariji waathirika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Miradi 17 ya maji safi, salama yatekelezwa miaka 3 ya Samia

**Na Elizabeth John,** MAKETE

MIRADI zaidi ya 17 ya maji safi na salama imetekelezwa wilayani Makete Mkoa wa Njombe na kusababisha kuwapo kwa huduma ya upatikanaji wa maji kufikia asilimia 91.6 wilayani humo. Hayo yameelezwa na Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda, wakati wa kikao cha wadau wa maji kilichofanyika wilayani hapa.

Alisema miradi hiyo ni kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan imekuwa na tija sana kwa wilaya yetu ya Makete na serikali katika kipindi hiki imeongeza miradi mingi ya maji ambapo kwa sasa maji yanapatikana kwa asilima 91.6 na malengo yetu ni kufikia asilimia 100," alisema Sweda.

Aidha, aliwashukuru wananchi wa Wilaya ya Makete kwa kuendelea kwa kutunza vyanzo vya maji sambamba na miradi mikubwa ambayo imejengwa kwenye maeneo yao.

"Niwapongeze sana wananchi wa Makete kwa kutunza vyanzo vya kwa ajili ya vizazi vya sasa na baadaye na serikali itaendelea kuboresha changamoto mbalimbali katika sekta ya maji ili muweze kunufaika," alisema Sweda.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Njombe, Seleman Mdaba alisema kuwa mkoa huo umeweka mpango kazi ambao utawafanya wakazi wote kufikiwa na maji safi na salama kwa bei nafuu. Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Wilaya ya Makete (RUWASA), Innocent Lyamuya alisema serikali imeendelea kuweka malengo ya kuboresha huduma za maji wilayani hapa.

Lyamula alisema serikali inalengo la kuhakikisha miradi ya maji vijiji inakuwa endelevu na kuhakikisha huduma ya maji inapatikana muda wote.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Makete, Christopher Fungo aliwataka viongozi wa kata kushirikiana na watendaji wa mamlaka ndogo za maji ili kutunza na kusimamia vyanzo vya sambamba na ukusanyaji wa ankara za maji kwa ufasaha kwa dhumuni la kuendeleza miradi ya maji iliyoletwa na serikali.

# NDC yawaita wawekezaji kutoka China kuwekeza katika miradi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Maendeleo (NDC) limewakaribisha wawekezaji kutoka China kuja kuwekeza nchini katika miradi mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo, uzalishaji wa madini ya viwandani pamoja na ujenzi wa kituo maalumu cha uzalishaji nishati jadidifu.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Sempeho Manongi, alitoa rai hiyo jana wakati wa kikao maalum kilichowashirikisha wawekezaji kutoka jimbo la Zhonglou China na maofisa wa NDC.

Alisema endapo Tanzania itapata wawekezaji katika maeneo ya nishati jadidifu itaongeza uzalishaji wa umeme pamoja na ajira kwa vijana.

"Jimbo la Zhonglou limeendelea katika uwekezaji wa viwanda. Hivyo hawa wenzetu wamekuja kuangalia fursa za uwekezaji katika uanzishaji wa viwanda vya kufunga na kuzalisha power tiller, vifaa vya trekta, vifaa tiba pamoja na viwanda vya kuzalisha vifaa vya umeme," alisema Manongi.

Naye ofisa kutoka kampuni ya Canopus Energy, Anna Nyangasi, alisema kampuni hizo kutoka China zinakuja kuwekeza katika uzalishaji wa mashine za kilimo (Dola za Marekani milioni 425).

Alisema pia wanakuja kuwekeza katika uzalishaji wa vifaa tiba (Dola za Marekani milioni sita), uzalishaji wa vifa vya umeme (Dola za Marekani milioni mbili), Uzalishaji wa vifaa vya ujenzi (Dola za Marekani milioni 11.3) pamoja na uzalishaii wa mafuta (Dola za Marekani milioni 43).

Katibu kutoka Chama cha kikomonisti kutoka China (CCP), Shen Dong, alisema uhusiano kati ya China na Tanzania ni wa kihistoria kwa sababu ulianza miaka mingi.

Alisema kampuni za China zimekuja Tanzania kuwekeza katika sekta ya kilimo, viwanda vya uzalishaji ikiwemo umeme, ujenzi na vifaa tiba.

Wawekezaji hao wameletwa nchini na kampuni ya AMEC group kwa kushirikiana na JINAKE group.



# Waziri aibana bodi mpya ya Taasisi ya Nyaraka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu, Ali Suleiman Mrembo, ameitaka Bodi ya Ushauri wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu kuhakikisha inafahamu jukumu la kusimamia taasisi hiyo.

Mrembo alitoa kauli hiyo juzi wakati akizindua bodi mpya ya taasisi hiyo huko Kilimani, akibainisha kuwa kwa miaka mingi hakukuwa na bodi, hivyo kuteuliwa kwao lazima wajue kuwa wanabeba jukumu muhimu.

Alisema nyaraka ni kitu muhimu katika nchi, hivyo watambue kuwa wanakwenda kuongoza taasisi yenye dhima muhimu na roho ya nchi.

Alisema ana imani kuwa ujuzi na uzoefu wao ndio sababu ya kuteuliwa kuwa wajumbe wa bodi, hivyo wahakikishe wanainua taasisi hiyo katika kufanya mabadiliko yenye tija kwa nchi.

Waziri huyo alisema ni vyema bodi hiyo ikapanga mipango ambayo serikali inahitaji hivi sasa kwa kuwa Taasisi ya Nyaraka ina majukumu makubwa.

Aliyataja majukumu hayo kuwa ni kutunza na kuhifadhi, hivyo bodi lazima ijue serikali inataka kuhifadhi nini na kipi kinapaswa kutunzwa.

Aliitaka bodi hiyo kushirikiana na taasisi nyingine za serikali katika kufanya kazi zao, ili kufikia malengo ya serikali ambayo imejipangia.

Waziri huyo pia alitaka bodi hiyo kuhakikisha ndani ya mwaka mmoja, ikamilishe ujenzi wa jengo la ofisi za nyaraka; ndani ya miezi sita msingi wake uwe umeshajengwa.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Ikulu, Saleh Juma Mussa, alisema lengo la kuundwa bodi hiyo ni kusaidia taasisi katika kutekeleza majukumu yake.

Alisema Taasisi ya Nyaraka ni moyo wa nchi, hivyo lazima iwe na nguvu ya kufanya kazi na ni vyema watumishi kwa upande wao wakaiunga mkono bodi hiyo.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Sheha Makame Mussa, alisema wanatambua kuwa wana jukumu kubwa la kuhakikisha taasisi hiyo inaendeshwa inavyopaswa.

Alisema atahakikisha mambo yote muhimu ambayo yanahitajika kuwapo kwenye taasisi yanapatikana, ikiwamo majina na picha za viongozi wote waliosimamia mapinduzi.

# Makamu wa Rais abaini jambo viongozi kutembelea wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ziara za kutembelea wananchi wenye matatizo katika maeneo wanamoishi ni muhimu na ni fursa kubwa kwa viongozi katika ngazi tofauti kujifunza na kujua hali halisi ya maisha waliyonayo.

Othman ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo aliyasema hayo jana Mkoa wa Kaskazini Unguja akiwa katika mwendelezo wa ziara ya kutembelea wagonjwa, wenye misiba na matatizo mbalimbali ya kijamii.

Alisema suala hilo linasaidia na linajenga matumaini ya kuwapo na kuendeleza umoja na mshikamano miongoni mwa viongozi na wananchi, pia kuwapa matumaini wananchi kwamba viongozi wako pamoja nao.

Alisema ni viongozi kujifunza kwa uhalisia changamoto za wananchi walizonazo sambamba na kutafuta mbinu za pamoja katika kuzikabili na kuzitatua changamoto hizo.

Othman alisema kufanya hivyo kwa viongozi ni kutekeleza wajibu mkubwa walionao katika kuwafariji na kuwapa matumini mema wananchi katika kuendeleza umoja miongioni mwa wananchi na viongozi wao kwa ngazi mbalimbali.

Pia alitaka wananchi na viongozi kuendeleza kuwa na umoja na subira kutokana na matatizo yanayowafika ikiwamo ni pamoja na magonjwa na misiba.

Aliagiza viongozi kuendeleza utaratibu huo wa kutembelea wananchi na wagonjwa hasa katika kipindi kama hiki cha Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Makamu wa Rais alisema ziara kama hizo ni alama za kuwakumbusha viongozi na wananchi wajibu wa kuwa pamoja wakati wa furaha na changamoto.

Othman alisema viongozi wamekabidhiwa dhamana na wananchi na wamekuwa wanafanya kazi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kusimamia vyema na kuwapo kwa matumaini ya kuondosha shida za wananchi kupitia serikali hiyo ili na wengine watamani kuiga mfumo wa serikali hiyo.

Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Mkoa wa Kaskazini A (kichama), Mcha Rajab Haji, alisema viongozi na wananchi wamefarijika kutokana na ziara za namna hiyo kwa kuwa zinawaweka pamoja.

Katibu wa Haki za Binaadamu na Makundi Maalum wa chama hicho, Pavu Abdalla Juma, alisema ziara hizo zinaleta faraja na matumaini kwa wananchi; viongozi wametembelea kaya 43 katika mkoa huo.

Alisema ziara hizo ni urithi ulioachwa na Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad ambaye katika uhai wake alizifanya kila ulipotimu Mwenzi Mtukufu wa Ramadhani, akitembelea wagonjwa, wenye misiba na shida nyingine katika visiwa vya Unguja na Pemba.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum akizungumza katika hafla ya utiaji saini wa ushirikiano na makubaliano kati ya kampuni ya Tigo Zantel na shirika la Bima Zanzibar kuhusu ukataji wa bima kwa vyombo vya moto kwa njia za kidijitali, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZIC, Tigo Zantel zaingia makubaliano bima kidijitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMPUNI ya Simu ya Tigo Zantel imeingia makubaliano ya ushirikiano na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kuhusu upatikanaji wa huduma za kifedha kupitia bima ya vyombo vya moto kwa njia ya kidijitali.

Akizungumza jana baada ya uzinduzi huo uliofanyika visiwani Zanzibar, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya alisema hatua hiyo ni njia bora kwa wamiliki wa vyombo vya moto kupata bima kupitia njia ya simu kwa urahisi.

Waziri huyo alisema hatua hiyo pia itasaidia kuondoa msongamano katika kituo kinachotoa huduma hizo za bima na mwananchi kupata huduma kupitia simu zao za mikononi.

Alisema Zanzibar inaendelea kutafuta njia za kuondoka katika huduma za kutumia karatasi na kutumia mifumo ya kidijitali ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi na kuendesha uchumi wa nchi.

Alisema ushirikiano huo kati ya Tigo na ZIC utasaidia serikali kufikia malengo yake ya kuwa na uchumi usio wa fedha taslimu.

"Mmekwenda haraka zaidi kuliko vile ambavyo tumepanga, hivyo angalieni ubunifu mwingine ambao utatuwezesha sisi kufikia malengo yetu kwa haraka zaidi," alisema Dk. Saada.

Aliongeza kuwa bado wananchi hawajaona umuhimu wa kuwa na bima, hivyo kuwataka kuendelea kutoa elimu huku serikali ikiendelea kutoa ushirikiano wa kisera na kisheria ili kuona sekta binafsi na sekta za umma zinasaidia maendeleo ya nchi.

Ofisa Mkuu wa Kampuni ya Tigo, Angelica Pesha, alisema ulimwengu wa sasa unaendana na teknolojia ambayo inahusishwa kwa karibu sana na maendeleo duniani kote, hivyo ushirikiano wao na ZIC ni hatua muhimu ya kuhakikisha Watanzania wanajumuishwa katika huduma za kifedha na za kidigitali ili kupata maendeleo.

Alisema kupitia bima ya vyombo vya moto ya Tigo Zantel wamewawezesha wateja wa Tigo wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kununua bima kwa ajili ya vyombo vya moto zikiwamo za magari, pikipiki na bajaji kupitia simu za mkononi.

Alisema ni asilimia 10 tu ya Watanzania wanatumia huduma za bima.

Mkurugenzi wa ZIC, Arafat Haji, alisema ushirikiano huo unakwenda sambamba na kuimarisha ufikiwaji huduma za bima na kuongeza ubunifu wa kurahisisha upatikanaji huduma ya bima kupitia simu ya mkononi.

Hivyo, alisema ushirikiano huo utafungua njia mpya zinazochochea ubunifu katika utoaji huduma nzuri na kuongeza thamani kwa wananchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**MONICA JEMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha **BACHELOR OF PUBLIC ADMINISTRATION** chenye usajili namba **BPA-RAM014440** kilichotolewa na **MZUMBE UNIVERSITY** mwaka 2014,cheti cha **DIPLOMA IN HUMAN RESOURCES MANAGEMENT** chenye usajili namba DC **NO.05339** kilichotolewa na chuo cha TPSC MAGOGONI mwaka 2011 na **CERTIFICATE IN COMMUNITY DEVELOPMENT** chenye usajili namba **BCC/CD NO.26/2024** kilichotolewa na **BUHARE CDTI** mwaka 2008. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/2099/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAGRETH ANTONY MSHANA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S0802-0014** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAKANYA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014, Cheti kimepotea mkoani Dar es Salaam. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **MBP/ RB/DOD/2539/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GAMALIEL RAYMOND KWEKA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 624 ALG BEDFORD.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taarifa : **PHQ/KIL/HAI/ 5636/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA PIKIPIKI

**RABIETH MBONEA MWERINDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 919 BUG** na kadi ya pikipiki yenye usajili namba **T 337 CTM.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/MUH/2632/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANI REGISTRATION OF DOCUMEMTS ACT (CAP 117)**
**CHANGE OF NAME**
**BY DEED POLL**

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made at Arusha this 28th day of December ,2023 by me THOMAS LOUIS PONSIAN formerly known as **THOMASLOUIS PONSIAN SEWANDO** of Post Office Box 1006,Arusha a resident of Tengeru, Arumeru District in Arusha Region now or until recently called **THOMAS LOUIS PONSIAN, and/or THOMASLOUIS PONSIAN SEWANDO:**


**WTTNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows:

1. **THAT, I** absolutely renounce, relinquish and abandon the use of my said former name of **THOMASLOUIS PONSIAN SEWANDO** in lieu thereof do assume as from the date hereof my new name of **THOMAS LOUIS PONSIAN** in substitution of my former name of **THOMASLOUIS PONSIAN SEWANDO,**
2. **THAT,IN PURSUANCE** of such change of name (s)as aforesaid **I DECLARE** that, I shall at all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of **THOMAS LOUIS PONSIAN** in substitution for my former name of ; **THOMASLOUIS PONSIAN SEWANDO**.so relinquished as aforesaid to the intent that,I may hereafter be known not by the aforesaid former name , but by the new name of **THOMAS LOUIS PONSIAN only ; AND**
3. **I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all persons at all times to describe and address me by the new name of **THOMAS LOUIS PONSIAN.**

**IN WTTNESS** whereof, I have hereunto subscribed my new name of **THOMAS LOUIS PONSIAN** and have affixed my signature the day and year herein written.

**SIGNED and DELIVERED** at Arusha by the said **THOMAS LOUIS PONSIAN** who is known to me personally/identified to me by .........the latter being known to me in presence this 29th day of DECEMBER 2023,

DEPONENT



BEFORE ME
Name: FRANK R. WILIAM
Signature:
Qualification: COMMISSIONER FOR OATH
Date: 29TH DEC. 2023.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6085 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late FRANK JOHN MDOTHA of Senje, Msalato Ward Ward within City Council of Dodoma.**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY STANSLAUS JOHN MDOTA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of The Probate Rules Gn 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 04, 2024
Dated at Kondoa this 15 Day of 02, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY:
PETITIONER
MAZIMBU WARD
P.O.BOX 5230
MOROGORO.

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

## Haiti bado hali ni tete

**PORT-AU-PRINCE,** Haiti

HALI ya kisiasa nchini Haiti bado iko mbaya baada ya Baraza la Mpito kushindwa kuunda serikali mpito.

Wajumbe wa baraza hilo walijikuta katika sintofahamu kutokana na kuibuka kwa malumbano miongoni mwa wajumbe kutoka vyama vya siasa. Wakati hayo yanajiri, mji mkuu wa Port-au-Prince unaendelea kutawaliwa na ghasia kwa wiki kadhaa.

Baraza hilo lenye wajumbe saba wa kupiga kura na wawili wasiopiga kura kutoka vyama vya siasa, sekta ya kibinafsi na makundi mengine. Moja ya kazi yake kubwa ni kumtangaza waziri mkuu wa mpito na serikali ambayo itaandaa mipango ya uchaguzi mpya.

Hadi jana wajumbe walishindwa kumchagua mwenyekiti wao baada ya kutoaminiana miongoni mwao.

Mkutano huo uliahirishwa hadi muda usiojulikana kwa sababu baadhi ya wawakilishi walijiuzulu nafasi zao. **DW**

## Mahasimu Sudan kukutana mwezi Aprili

**KHARTOUM,** Sudan

MJUMBE maalum wa Marekani nchini Sudan, Tom Perriello, amesema kuna matumaini mazungumzo ya kutafuta amani yatafanyika tena baada ya kumalizika kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Perriello, alithibitisha kuwa mazungumzo hayo yataendelea tena Aprili 18, chini ya usimamizi wa nchi za Marekani na Saudi Arabia.

Aidha, amesema hakuna mshindi kati ya jeshi la serikali na wanamgambo wa RSF, akisisitiza uwepo wa umuhimu wa kufanyika kwa mazungumzo hayo.

Kumekuwa na jitihada za kuendeleza mazungumzo hayo yaliyoandaliwa katika mji wa Pwani wa Jedda nchini Saudi Arabia. **RFI**

# Marekani yaikasirikia Israel kuhusu ulinzi wa wapalestina

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, amesema ni suala la kimaadili na kimkakati kuwalinda raia wa Kipalestina katika vita vinavyoendelea kati ya Israel na Hamas.

Kauli hiyo ya kiongozi wa juu wa Marekani ilitolewa wakati wa mkutano wake na Waziri wa Ulinzi wa Israe, Yoav Gallant, uliofanyika makao makuu ya ulinzi ya Pentagon.

Uhusiano kati ya Rais wa Marekani Joe Biden na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, unaonekana kutetereka kila siku kutokana na kila upande kuwa na msimamo tofauti.

Baada ya mkutano huo, Waziri wa ulinzi wa Israel alikutana na mshauri wa usalama wa taifa, Jake Suillivan, ambaye alimwambia Gallant kuwa Israel inahitajika kuongeza msaada wa kiutu Ukanda wa Gaza.

**Kwa upande wa Marekani, ilisema ndege mbili aina ya C-17 zilitumika kudondosha chakula kilichokuwa tayari kilo 46,000.**

Katika ziara yake, Gallant alikutana na mkurugenzi mkuu wa shirika la Upelelezi la Marekani (CIA), William Burns, ambaye aliyerejea kutoka kwenye mazungumzo ya amani yaliyofanyika nchini Qatar.

Wakati wa mkutano na waandishi wa habari, Waziri wa ulinzi wa Israel. Alijaribu kutuliza mivutano kati ya nchi yake na Marekani kwa kueleza kuwa uhusiano wao uko imara kwa ajili ya usalama wa nchi yake na kulitengeneza jeshi la Israel kuwa bora zaidi katika kanda hiyo.

Rais Biden amejikuta akiwa chini ya shinikizo kali kutoka kwa makundi ya haki za binadamu na baadhi ya wanachama wa Democratic wenzake wanaomtaka kuweka masharti makali kabla ya kutolewa msaada zaidi wa kijeshi kwa Israel.

Wakati huo huo, serikali ya Gaza inayoongozwa na Hamas ilisema Wapalestina 18 wameuawa walipokuwa wakijaribu kukusanya misaada kaskazini mwa Gaza.

Watu 12 walikufa wakati walipoingia baharini kuchukua vifurushi vya chakula na wengine sita walikufa katika mkanyagano wakati wakigombea vifurushi vya misaada vilivyotupwa kwa kutumia ndege.

Serikali hiyo ilitaka kusambaza misaada kwa kutumia njia anga ikomeshwe na kuiita kama inayokera na isiyofaa.

Video, iliyochukuliwa na shirika la habari la Reuters, iimeonyesha jinsi Wapalestina walivyokuwa wakikimbilia pwani baada ya misaada kuangushwa kwenye ufuo karibu na mji wa Beit Lahia juzi.

Hata hivyo serikali ya ilisema iliwezesha vifurushi vya tani 159 za misaada kuingizwa kaskazini mwa Gaza siku hiyo.

Kwa upande wa Marekani, ilisema ndege mbili aina ya C-17 zilitumika kudondosha chakula kilichokuwa tayari kilo 46,000.

Uingereza nayo ilieleza moja ya ndege zake aina ya A400M ilidondosha tani 10 za maji, mchele, mafuta ya kupikia, unga na vinywaji vya Watoto.

Mashirika ya kibinadamu yameonya kuwa misaada inayorushwa kwa njia hiyo haiwezi kukidhi hitaji kubwa la chakula. **DW**



Raia wa Palestina wakipita katika eneo lililobaki magofu baada ya nyumba kubomolewa katika mashambulizi yanayofanywa na jeshi la Israel katika Ukanda wa Gaza juzi. **PICHA: REUTERS**

# Russia yalaumu Marekani, Ulaya kuwasaidia magaidi

**MOSCOW,** Marekani

MAOFISA wakuu wa serikali ya Russia wameishutumu moja kwa moja Ukraine na nchi za Magharibi kwa kuhusika katika shambulio lililouwa watu zaidi ya 100 kwenye ukumbi katika jiji la Moscow.

Kundi la Islamic State (IS) lilidai kuhusika na tukio hilo kwa maelezo kulipiza kisasi.

Licha ya IS kutoa video ikionyesha shambulio hilo, Rais wa Russia Vladimir Putin na washirika wake wawili walidai wanajihadi hao walisaidiwa na mashirika ya ujasusi wa nchi za Magharibi na Ukraine.

Ukraine ilikana kuhusika na shambulizi hilo na kueleza madai ya Russia ni ya uongo.

Siku 15 kabla ya tukio hilo, Marekani ilitoa onyo kuhusu shambulio hilo.

Russia ilisema watu 139 waliuawa wakati watu wanne waliokuwa na silaha walipovamia ukumbi unaofanyika matamasha unaoitwa Crocus City Hall, Ijumaa jioni.

Watu wengine 22 wanaendelea kupatiwa matibabu kutokana na hali zao kuwa mbaya.

Raia wanne wa Tajikistan walifikishwa mahakamani wakituhumiwa kutekeleza mauaji hayo.

Washukiwa wengine wanne wameshtakiwa kwa kusaidia ugaidi.

Mshauri wa rais wa Ukraine, Mykhailo Podolyak, alisema ukweli kuhusu wahalifu huo unatokana na udhaifu wa vyombo vya usalama za Russia na hilo halipingiki.

Rais Putin wakati akizungumza kupitia televisheni alikiri kwamba nchi za Magharibi ziko nyuma ya shambulizi hilo.

"Tunajua uhalifu ulifanywa na Waislam wenye itikadi kali, tunataka kujua ni nani aliyeamuru." Alisikika akihoji. **BBC**

HABARI MICHEZO

# RUN FOR BINTI MARATHON RASMI KUFANYIKA MEI 25

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Smile for Community (S4C) kwa kushirikiana na Legal Services Facility (LSF) limetangaza kuandaa msimu wa tatu wa mbio za Run for Binti zitakazofanyika Mei 25, mwaka huu jijini, Dar es Saalam.

**Mbio za Run for Binti zinazoratibiwa kila mwaka zina lengo la kuweka nguvu na raslimali za pamoja katika kuwawezesha watoto wa kike kupata haki ya elimu na afya ya uzazi kwa kuhakikisha wanapata hedhi salama , mazingira bora ya kusoma.**

Kupitia mbio hizo mwaka jana, wanafunzi wa Shule za Sekondari Nanyamba na Chawi za Halmashauri ya mji Nanyamba walinufaika na kujengewa vyoo bora huku wanafunzi wa kike wakipata taulo ili kulinda afya zao pamoja na kuhudhuria vipindi darasani bila kukosa.

Akizungumza jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema "Katika utekelezaji wa mradi wetu wa upatikanaji wa haki nchi tumeona dhahiri wasichana na mabinti wadogo wanakabiliana na vizuizi visivyoweza kuzuilika na vinavyozuilika katika kupata elimu, huduma za afya na haki zao za msingi.

Ndio maana LSF tukaona ni vyema mashirikiano hayo na Smile for Community pamoja na wadau mbalimbali ni muhimu katika tunapunguza vikwazo na kutengeneza njia mpya itakayochochea kuwa na jamii yenye haki na usawa hususani kwa watoto wa kike," alisema Ngwanakilala.

Aliongeza mbio hizo za Run for Binti tangu zilipoanzishwa zimekuwa na tija katika kuwaleta wadau pamoja kwa kuweka rasilimali fedha na nguvu ya pamoja kwenye kutatua changamoto za jamii.

Alisema mbio za mwaka jana zimewezesha ukaratabi na ujenzi na miundombinu ya vyoo na usambazaji wa taulo za kike na utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti katika shule mbalimbali na wanafunzi zaidi ya 2,500 kunufaika katika shule za Sekondari za Mtwara.

Aliongeza pia mbizo hizo zimesaidia utoaji wa elimu na kuongeza uelewa kwa jamii juu haki ya afya na hedhi salama pamoja na kushughulikia ukatili wa kijinsia unaowakumba watoto na kupelekea kupata mimba za utotoni ambazo hukatisha.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Smile for Community, Flora Njelekela, alisema kwa kushirikiana na LSF alieleza wanariadha watachuana katika mbio za kilomita 21, kilomita 10 na kilomita tano huku pia kutakuwa na mbio za baiskeli za kilomita 55.

"Sisi Smile for Community waanzilishi wa mbio hizi tunaona fahari kuiwezesha jamii katika maeneo ya pembezoni kupata elimu ya afya ya uzazi na hedhi salama lakini kupata elimu endelevu ambayo kama taasisi tumekuwa tukiitekeleza kupitia miradi yetu mbalimbali na pia kupitia mbio hizi za Run for Binti kila mwaka," alisema Njelekela.




Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala (kulia) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Smile Community, Flora Njelekela, wakati wa Uzinduzi wa Msimu wa Tatu wa Mbio za Run For Binti zinazotarajiwa kufanyika Mei 25, mwaka huu kwenye viwanja vya Oysterbay jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Singida Fountain Gate yajinoa ufukweni*

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha kikosi chake kinakuwa imara kwa ajili ya kusaka matokeo chanya katika hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara, timu ya Singida Fountain Gate, inafanya mazoezi maalumu ufukweni, imeelezwa.

Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Jamhuri Kihwelu 'Julio' aliliambia gazeti hili wachezaji wake wanafanya mazoezi kwenye ufukwe wa Bamba ulioko Kigamboni, Dar es Salaam na anaamini programu hiyo itawasaidia kuwajenga na kuiweka sawa miili yao.

"Haya mazoezi ambayo ninawapa yatawasaidia kufanya vizuri katika mechi zetu zinazofuata za msimu huu, kwa sasa sina muda wa kupoteza, " alisema Julio.

Kocha huyo alisema tangu waanze mazoezi hayo hapo juzi kila mchezaji ameonyesha morali yake na anaamini yatawasaidia kufikia malengo yao.

Naye daktari wa timu hiyo, Shabani Shija, alisema hali za wachezaji waliokuwa majeruhi zinaendelea kuimarika.

"Ninashukuru afya za wachezaji wangu zinaendelea vyema ingawa wapo baadhi yao jana (juzi), walipata maumivu makali kutokana na aina ya mazoezi wanayopewa, ila kila kitu kitaenda sawa," alisema Shija.

Daktari huyo alieleza wachezaji hao wamepata kwa sababu miili yao imetoka katika mapumziko mafupi na amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kwa kusema hiyo ni hali ya kawaida.

## Dulla Mbabe kamili kumchapa Simpson

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Pazi 'Dullah Mbabe' amesema yuko tayari kwa ajili ya pambano lake la kimataifa lisilo la ubingwa dhidi ya Callum Simpson kutoka Uingereza litakalofanyika Jumapili, imeelezwa.

Pambano hilo litakuwa la raundi 10 na lifanyika kwenye Ukumbi wa O2 Arena, Greenwich jijini, London.

Dullah aliliambia gazeti hili anaenda katika pambano hilo akiwa na kumbukumbu nzuri ya kushinda mchezo wake wa mwisho wa dhidi ya Mmalawi, Limbani Lano.

Alisema kama bondia muda wote anapaswa kuwa fiti ili aweze kucheza mapambano mengi na kutwaa mikanda hivyo amejiandaa kupanda ulingoni katika kwenye ubora mkubwa.

"Kazi yangu ni ngumi na kuwafanya wapenzi wa ngumi wafurahi ndio maana najifua ili niweze kushinda kila pambano lililo mbele yangu, ingawa siwezi kumzungumzia mpinzani nitakaye kutana naye," alisema bondia huyo.

## Wanariadha mbio za Nyika waahidi medali

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA wanne watakaoiwakilisha Tanzania katika mashindano ya riadha ya mbio za Nyika yatakayofanyika keshokutwa nchini Serbia wameondoka nchini wakiwa na matumaini ya kwenda kupeperusha vyema bendera ya nchi, imeelezwa.

Rais wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Silas Isangi, alisema wanariadha hao wameondoka lakini chama kinaamini watafanya vyema katika mashindano hayo kutoka na maandalizi waliyofanya.

Isangi alisema wanariadha hao waliondoka mapema ili kwenda kuzoea hali ya hewa katika mashindano hayo yanayoshirikisha vijana wenye umri kati ya miaka 17 na 20.

"Tumeamua kuwapeleka mapema ili wakazoee hali ya hewa pamoja na mazingira ya mchezo, lengo letu tunataka warudi nyumbani na medali za ushindi," alisema Isangi.

Aliongeza mashindano hayo yatakuwa na upinzani mkubwa kutokana na kushirikisha wanariadha vijana huku akiishukuru serikali kwa kusimamia maandalizi ya wanariadha wa Tanzania.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### YAMTOLEA MACHO HAALAND

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Norway, Erling Haaland (23) anasakwa na Barcelona katika msimu wa joto wa 2025. Wakala wa mchezaji huyo, Rafaela Pimenta, alikutana na mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo ya LaLiga, Deco, mwezi uliopita. ***(Mundo Deportivo)***

### TONEY ANUKIA MAN UNITED

MSHAMBULIAJI wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuwa chaguo kwa Manchester United msimu huu wa joto. ***(Fabrizio Romano kupitia Caught Offside)***

### MBADALA WA CASEMIRO

MANCHESTER United wamemtambua kiungo wa kati wa Wolves na Brazil, Joao Gomes mwenye umri wa miaka 23, kama mbadala wa Casemiro mwenye umri wa miaka 32. ***(Sport)***

### ISAK KUTUA ARSENAL

ARSENAL inaonekana kuimarika katika nafasi yao ya kumsajili mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kukiri "mambo yanaweza kutokea" katika dirisha la usajili. ***(Mail)***

### AFIKIRIWA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kumnunua mlinzi wa kati wa Sporting Lisbon na Ivory Coast, Ousmane Diomande mwenye umri wa miaka 20. ***(Sun)***

### MAN UNITED NA SOUTHGATE

MANCHESTER United italeta kikosi kizima cha kiufundi cha England ikiwa watamteua Gareth Southgate kama kocha wa Klabu hiyo katika msimu wa joto. ***(Sun)***

### MOURINHO KUREJEA KAZINI

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amesema yuko tayari kurejea kufundisha msimu huu wa joto kufuatia kuondoka kwake kutoka AS Roma. ***(Fabrizio Romano)***

### DE ZERBI AGEUKA LULU

PAMOJA na wote wanaomtaka kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, Liverpool na Bayern Munich wanamtaka kocha wa Brighton, Roberto de Zerbi kama mbadala wake. ***(Bild)***


### BABA WA LUIS DIAZ ANENA

BABA yake Luis Diaz amesema "tumaini bado halijapotea" kuhusu winga huyo wa Liverpool wa Colombia mwenye umri wa miaka 27, anayecheza Hispania. ***(Cadena SER)***

### ADAMS KUTUA WOLVES

KLABU ya Wolves inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Southampton na Scotland, Che Adams mwenye umri wa miaka 27, atakapokuwa mchezaji huru msimu wa joto. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RAPHINHA HATAKI KUONDOKA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

WINGA wa Barcelona, Raphinha 'amechanganyikiwa' na maisha ya klabu hiyo, ripoti imedai, lakini amedhamiria kubakia hapo Camp Nou baada ya msimu huu wa joto.

**Raphinha amekuwa akihusishwa na kuondoka Barcelona huku klabu hiyo ikitaka kumuuza ili ipate fedha, huku Ligi Saudi Arabia ikitajwa kuwa na nafasi za kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.**

Kwa mujibu wa Sport, kuhusishwa mara kwa mara na klabu nje ya Barcelona kumemwacha Raphinha akijihisi kuchanganyikiwa, kwa sababu anajua kuna ukweli katika suala hilo.

**Nyota huyo amekuwa akihusishwa kuondoka klabuni hapo huku Wahispania hao...**

Raphinha anasemekana kuamini kwamba hapati uungwaji mkono kamili wa mashabiki, bodi ya klabu hiyo na waandishi wa habari wa Hispania, hadi kufikia kuhisi kana kwamba hajawahi kuungwa mkono tangu kuhamia kwake kwa gharama kubwa katika klabu hiyo majira ya joto mwaka 2022.

Licha ya kutajwa kwamba atauzwa, Raphinha amesisitiza kuwa bado ana mustakabali Barcelona na hayuko tayari kutafuta klabu mpya.

Raphinha amekosa nafasi ya kuanza mara kwa mara chini ya Xavi msimu huu na amemaliza dakika 90 mara mbili tu kwenye LaLiga, na anaamini kwa sababu hiyo kwamba wale wanaoiongoza Barcelona wana nia ya kumuuza ili kupata fedha.

Barcelona wanataka zaidi ya euro milioni 80 ili kuachana na Raphinha, lakini hawatarajiwi kupokea kiwango hicho cha maslahi kutoka klabu za Ligi Kuu England ambapo Arsenal na Tottenham Hotspur wamehusishwa kutaka kumnunua winga huyo wa zamani wa Leeds United.

Klabu za Saudi Arabia zinatarajiwa kumpiga bei Raphinha, lakini kwa hali ilivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil hana nia ya kuondoka ama Barcelona au Ulaya.

## HABARI MICHEZO

# JERAHA LA ROBERTSON LAMPASUA KICHWA KLOPP



**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa kushoto wa Liverpool, Andy Robertson alionekana kuchechemea wakati wa kipindi cha kwanza kwenye mchezo ambao Scotland walikutana na Ireland Kaskazini juzi baada ya kupata jeraha la kifundo cha mguu.

Robertson alipata jeraha baya la bega wakati wa mapumziko ya kimataifa ya Oktoba mwaka jana hali iliyomfanya kuwa nje ya uwanja hadi Januari na sasa atakuwa akihofia kuwa nje ya uwanja tena.

Nyota huyo wa Liverpool alionekana ameshikilia kifundo cha mguu wake baada ya kugongana na Trai Hume wa Sunderland na alionekana kutokuwa na raha wakati akitoka uwanjani.

Kocha wa majogoo hao, Jurgen Klopp atakuwa akitoa jasho juu ya utimamu wa Robertson kabla ya Liverpool kurejea uwanjani Machi 31 kuwakabili Brighton & Hove Albion.

Iwapo Robertson atahitaji muda wa kuwa nje, Klopp anaweza kuwageukia Kostas Tsimikas au Joe Gomez, ambaye alifurahia uchezaji bora wa Robertson mapema msimu huu.

Darwin Nunez, ambaye alifunga bao la aina yake kabla ya mapumziko ya kimataifa, hakusafiri na Uruguay na anatarajiwa kurejea uwanjani hivi karibuni.

Kiungo Curtis Jones pia anaweza kuwa tayari kucheza dhidi ya Brighton, lakini Trent Alexander-Arnold na Diogo Jota wanaweza kuhitaji muda wa ziada nje ya uwanja, ingawa Klopp amethibitisha kuwa anawatarajia wote wawili kurejea wiki ijayo.

# *Man Utd yamtaka O'Neil kumrithi Hag*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inataka kuzungumza na kocha mkuu wa Wolverhampton Wanderers, Gary O'Neil kuhusu jukumu katika mpango mpya wa ukocha wa Old Trafford, vyanzo vimeiambia ESPN.

Huku kundi la Sir Jim Ratcliffe la Ineos sasa likisimamia shughuli za soka huko United baada ya kukamilika kwa ununuzi wao wa asilimia 27 ya hisa za klabu Februari, vyanzo vimesema kuwa utawala huo mpya, unaoongozwa na mkurugenzi wa michezo wa Ineos, Sir Dave Brailsford, unajaribu kujenga muundo mpya wa kufundisha.

Na ingawa hakuna uamuzi wa mwisho ambao umefanywa kuhusu hatma ya Erik ten Hag kama kocha, vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United tayari imemtathmini kocha wa England, Gareth Southgate, bosi wa Brighton, Roberto De Zerbi na Thomas Frank wa Brentford kama warithi wanaotarajiwa.

O'Neil, ambaye aliteuliwa kuwa kocha Molineux Agosti mwaka jana baada ya kuondoka kwa Julen Lopetegui, ameiwezesha Wolves kufuzu michuano ya Ulaya msimu huu baada ya kuibakisha Bournemouth kwenye Ligi Kuu England wakati wa kazi yake ya kwanza ya ligi kuu msimu uliopita.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba, kocha huyo mwenye umri wa miaka 40 amefahamishwa kuhusu nia ya United, huku viongozi wakuu wa klabu wakieleza nia ya kujadili mpango huo.

Vyanzo vimethibitisha nia ya United kwa O'Neil kwa ESPN, ingawa jukumu ambalo wanaweza kuwa tayari kutoa halijulikani.

Pamoja na kutathmini chaguzi za usimamizi, vyanzo vimesema United pia inaangalia kuimarisha benchi lao lote la ufundi.

O'Neil alitia saini mkataba wa miaka mitatu alipokuwa akiinoa Wolves msimu uliopita wa joto, akiiacha United ikiwa na matarajio ya kulipa fidia iwapo wataamua kumpa kazi katika klabu hiyo.



# Manchester City majeruhi kibao ikiikabili Arsenal

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER City ilimtazama John Stones akichechemea baada ya kuumia wakati wa mechi ya kirafiki ya England dhidi ya Ubelgiji, Jumanne na kumfanya kuwa mlinzi wa nne kupata majeraha.

England ilikuwa tayari bila Kyle Walker, ambaye alipata tatizo la msuli wa paja wiki iliyopita, huku Stones akionekana kunyoosha misuli alipoteleza uwanjani kwenye mchezo huo.

Mapumziko ya kimataifa ya Machi hayakuwa ya fadhili kwa City ambao katikati ya majeraha ya nyota hao wa England, pia walimtazama beki wa kati wa Uswisi, Manuel Akanji akikosa mchezo wa Jumanne dhidi ya Jamhuri ya Ireland kutokana na kuwa majeruhi.

Kocha Pep Guardiola ataumiza kichwa wakati City ikimenyana na Arsenal mnamo Machi 31 katika mechi ambayo inaweza kuwa suluhu katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu ya England, na huenda akalazimika kukabiliana na mchezo huo bila mabeki watatu chaguo la kwanza.

Ederson, Jack Grealish na Kevin De Bruyne wote walikosa kuitwa kwa sababu ya masuala ya utimamu wa mwili, wakati mshambuliaji Erling Haaland alionekana kuumia kwenye mazoezi ya Norway.



HABARI MICHEZO

# SIMBA YAFUNGUKA HATIMA YA PHIRI, ATAKIWA AJITUME

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema nyota, Moses Phiri, bado ni mchezaji wa timu yake kwa sababu ana mkataba wa zaidi ya mwaka mmoja na alipelekwa kwa mkopo katika klabu ya Power Dynamos ya Zambia.

Simba imesema hayo baada kuwapo na maswali mengi juu ya kuachwa kwa mshambuliaji huyo katika kipindi cha dirisha dogo na Wekundu hao wa Msimbazi wakiwasajili, Freddy Michael na Pa Omar Jobe.

**Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema Phiri ni mchezaji halali wa Simba na alipelekwa kwa mkopo Power Dynamos kwa ajili ya kurejesha ubora wake na endapo ataimarika atarejea Msimbazi.**

Kajula alisema uamuzi wa kumtoa kwa mkopo Mzambia huyo ulitokana na mapendekezo kutoka katika benchi la ufundi na hiyo ni hali ya kawaida pale mchezaji anaposhuka kiwango.

"Phiri ni mchezaji wetu halali ana mkataba wa mwaka moja, amepelekwa kwa mkopo Power Dynamos kwa lengo la kupata nafasi ya kucheza na kurudi katika ubora wake," alisema Kajula.

Aliongeza baada ya nyota huyo kukosa namba katika kikosi cha kwanza baada ya kupona majeraha, alitakiwa kupambana ili kurudi kwenye ubora wake na kuisaidia timu hiyo.

Kajula aliwataja nyota mbadala wa Phiri waliosajiliwa ni Freddy na Pa Jobe ambao nao wanatakiwa kupewa muda wa kuzoea mazingira.

Simba inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwakaribisha Al Ahly katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Wachezaji wa Simba Queens wakishangilia baada ya kufunga bao katika mechi ya kirafiki dhidi ya Kinondoni Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, Dar es Salaam hivi karibuni. Simba Queens ilishinda mabao 14-0. **PICHA: SIMBA SC**

## Mao atoa somo, Stars ikirejea

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kimerejea nchini jana alfajiri kikitokea Azerbaijan, ambapo ilishiriki mashindano maalum ya FIFA Series 2024, huku kiungo mkongwe, Himid Mao, akiwaasa wachezaji vijana kupambana na kulinda viwango vyao kwa sababu nchi inawategemea kuelekea katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), pamoja na AFCON ijayo.

Ikicheza kwenye Uwanja wa Dalga, Stars ilianza michuano hiyo kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Bulgaria na mchezo wa pili iliwachapa Mongolia mabao 3-0.

Akizungumza wakati wa kuwaaga wachezaji wenzake, Himid, aliwataka wachezaji vijana kuendelea kupambana wanapokuwa katika timu zao ili kulinda viwango vyao kwa ajili ya kuisaidia Stars inayokabiliwa na michuano mbalimbali hivi karibuni.

"Wachezaji wenzangu napenda sana kuwashukuru wote, tunathamini sana mchango wa kila mmoja, kama unavyoona timu yetu imekuwa na vijana wadogo, wanahitaji sana uwepo wetu sisi wakongwe.

Tutaendelea kuwasapoti ili wafanye vizuri, sapoti yetu itawafanya waendelee kupambana hata wanapokwenda katika klabu zao wajiamini, wafanye vizuri kwa sababu taifa linawahitaji sana kwenye michuano mbalimbali inayokuja,' alisema mchezaji huyo wa zamani wa Azam FC ambaye sasa anaichezea Tala'ea El Gaish SC ya Misri.

## *Yanga: Tutaishangaza Afrika michuano CAF*

INATOKA UKURASA 24

na ya utani wa jadi.

Kamwe alisema licha ya kutangaza kuingia bure katika eneo la mzunguko, lakini ulinzi utakuwa mkali, hivyo wamewataka mashabiki wasiogope kuminika uwanjani.

"Msiwe na wasiwasi, mje ulinzi utakuwa mkali, ila tunachotaka kuwaambia wanachama na mashabiki wa Yanga, mechi hii itakuwa na mashabiki wengi kutoka mataifa mengi mbalimbali, hivyo kila mmoja akiwa uwanjani, ahakikishe anajali usalama wa mwenzake," alisema ofisa huyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa Yanga kucheza hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa tangu kuanza kwa muundo huo mwaka 1997, huku ikiwa imejidhatiti kusonga mbele.

Baada ya mechi ya keshokutwa, timu hizo zitakutana Afrika Kusini katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Aprili 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Loftus Versfield ulioko Pretoria.

Yanga bado inashiriki mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ikiwa na kumbukumbu ya kucheza fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita, ilipoteza dhidi ya wenyeji USM Alger ya Algeria.

## Simba SC waitwa kuandika historia

INATOKA UKURASA 24

"Huu ni mchezo muhimu sana kwetu, tunatakiwa kufanya kila linalowezekana ili kupata ushindi mkubwa hapa nyumbani. Ukicheza na timu (Al Ahly) kama hii unatakiwa kutumia vizuri kila nafasi utakayoipata kwa sababu ni wazoefu, hawawezi kukuruhusu kutengeneza nafasi nyingi sana.

Kutokana na hali hiyo, ninaendelea kuwafua washambuliaji wangu, ninawasisitiza kila nafasi lazima tuitumie vizuri, tunatakiwa kumaliza mchezo hapa nyumbani, tukipata ushindi wa idadi kubwa ya mabao itakuwa ni faida kubwa sana kwetu," kocha huyo alisema.

Aliongeza ili kuisuka vyema safu yake ya washambuliaji, ameendelea kuwapa mbinu tofauti tofauti sambamba na nyota wake wanaocheza eneo la ulinzi kuhakikisha hawaruhusu bao kwa sababu inaweza ikawagharimu mbele ya safari.

"Sio nahangaika na safu ya ushambuliaji peke yake, hapana, pia nimekuwa nikitumia muda mwingi kuikumbusha safu ya ulinzi hawatakiwi kufanya kosa lolote, kama safu ya ushambuliaji watakuwa wanafunga halafu safu ya ulinzi inaruhusu mabao kizembe itakuwa ni kazi bure," alisema kocha huyo.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi kilipokuwa Zanzibar, kilifanya mazoezi maalum katika kila idara ili kuboresha viwango vya wachezaji wao.

Ahmed alisema kipindi chote cha siku nane, kocha (Benchikha), alitenga muda wa mazoezi wa kila eneo kwa kuwapa mbinu za kukabiliana na Al Ahly.

"Zoezi hilo linaendelea, kikosi kina mabadiliko makubwa ya ubora katika idara zote, hatuna mashaka kabisa na eneo la ushambuliaji, kocha ameongeza makali," alisema Ahmed.

Aliongeza wachezaji wote wako fiti huku kiungo Clatous Chama akiwa ameingia kambini jana moja kwa moja ili kujiunga na wenzake kuendelea na maandalizi ya kuwavaa Al Ahly.

"Mwaka huu tumedhamiria kumwondoa Al Ahly, Wanasimba sasa ni muda wao wa kujitokeza kwa wingi uwanjani ili kuwa sehemu ya historia ya kumwondoa Al Ahly na Simba kuingia nusu fainali," alimaliza meneja huyo.

# Michezo

Alhamisi Machi 28, 2024
Nipashe




Jeraha la Robertson lampasua kichwa Klopp UKURASA 22




Mashabiki wa Simba kutoka sehemu mbalimbali jijini, Dar es Salaam jana wakihamasisha kuelekea mechi ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MTANDAO**

## Simba: Mashabiki njooni tuandike historia mpya

**Na Saada Akida**

MABAO, mabao, mabao, hicho ndio kilio cha Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, kuelekea mechi ya robo fainali Afrika dhidi ya Al Ahly itakayochezwa kesho kwa kuwapa mbinu mpya safu yake ya ushambuliaji ili kuhakikisha wanapata ushindi na si matokeo mengine tofauti, imefahamika.

Simba watakuwa nyumbani kwenye dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kesho kuwakaribisha Waarabu hao wa Misri katika mchezo wa kwanza wa robo fainali wa Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa kuanzia saa 3:00 usiku.

Benchikha ameliambia Nipashe anataka kuona washambuliaji wake wanatumia vizuri kila nafasi watakayoipata katika mechi hiyo ili kumaliza 'kazi'.

ili kufikia malengo, kocha huyo ameamua kuifua upya safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa na Fredy Michael, Pa Jobe Omar na Mtanzania Kibu Denis, kwa kuwakumbusha kuongeza umakini katika mechi hiyo itakayowatengenezea historia mpya.

Kocha huyo amesema hataki kuona nyota wake wanapoteza nafasi kizembe kwa sababu mchezo huo ni wa maamuzi na wanahitaji kumaliza safari waliyoianza mapema.

Aliongeza malengo yake ni kuhakikisha kikosi hicho kinapata ushindi mnono na ili kufikia hapo, amelazimika 'kuvaa sura ya kazi' kwa kuwasisitiza wachezaji wake kujituma na kucheza kwa nidhamu wakifahamu wanacheza na moja ya timu ngumu Afrika.

Kocha huyo ambaye msimu uliopita aliipa ubingwa wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, USM Alger ya Algeria alisema anataka kuiona Simba ikipenya na kutinga hatua ya nusu fainali na hilo litafanikiwa endapo washambuliaji watazitendea haki nafasi watakazopata.

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga: Tutaishangaza Afrika

## ●●● Vinara hao wa Ligi Kuu Bara watamba wanataka kuonyesha ukubwa wao...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya watangazaji na wachambuzi wa soka mbalimbali kutoipa Yanga nafasi ya kufanya vizuri katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini, uongozi wa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara umesema wataishangaza Afrika.

**Yanga itawakaribisha Mamelodi Sundowns katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.**

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jana mazoezi ya timu yake yanayoongozwa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, yanawapa matumaini ya kuondoka na matokeo chanya katika mechi hiyo muhimu.

Kamwe alisema kikosi chao kipo tayari kuwavaa Mamelodi Sundowns na wanaamini watapata ushindi katika mchezo huo.

Alisema benchi la ufundi limekamilisha kila kitu kinachohitajika kuanzia kiufundi na kimbinu ili kupata ushindi, na kwa sasa wanasubiri kuona wachezaji wanafanya kile walichowaelekezwa kwenye uwanja wa mazoezi.

"Tangu Yanga imepangwa na Mamelodi Sundowns kwenye droo, nimeona watangazaji na wachambuzi hapa nchini na Afrika kwa ujumla kama vile hakuna kitu chochote kizuri ambacho timu yetu imefanya. Wao wanachokijua ni mambo mazuri ya wapinzani wetu, wanachofanya ni kuwataja wachezaji wazuri tu wa Wasauzi hao, kama vile sisi hatuna wachezaji bora.

Sasa tunawaambia tutakachowafanya Mamelodi hawataamini, ujumbe wa Jumamosi utakwenda kwa wote ambao hawaamini kama sisi tunaweza kuifunga timu hiyo, tunakwenda kuwaonyesha kuwa sisi ni wakubwa na tutaishangaza Afrika," alisema Kamwe.

Hata hivyo, wakati Yanga ikiendelea na hamasa, Kamwe amesema ameambiwa na Rais wa Yanga, Hersi Said, mwisho wa hamasa ni Alhamisi (leo), kwa ajili ya kupisha mechi nyingine ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kati ya wawakilishi wengine wa Tanzania, Simba dhidi ya Al Ahly ya Misri.

"Rais wa Yanga ameniambia tufanye hamasa kuanzia Jumanne, Jumatano na Alhamisi iwe mwisho, tuache Ijumaa na wenzetu nao wajulikane kama wamo na wana mechi kwa sababu hawajadiliwi, Afrika nzima inazungumza mechi hii (Yanga na Mamelodi Sundowns) na siyo yao," alisema Kamwe kwa nam-




Mashabiki wa Yanga kutoka sehemu mbalimbali jijini, Dar es Salaam jana wakihamasisha kuelekea mechi yao ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns itakayofanyika keshokutwa. **PICHA: MTANDAO**

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >